ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 19 Januari, 2011

(Kikao Kilianza saa 3:00 Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani nakala zote za Gazeti rasmi la Serikali pamoja na vijazo vyake kuanzia tarehe 12 Novemba mwaka 2010 naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Hebu ngoja. Nataka niangalie kama kuna mtu ana suali juu ya nakala hiyo, hakuna.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu marekebisho ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati wa Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria Utawala kuhusu marekebisho ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 5

Ujenzi wa Jengo la Afisi ya Baraza laWawakilishi

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza**:-**

Kukamilika kwa jengo la aina yake la Baraza la Wawakilishi na kwa kiwango cha hali ya juu, ni jambo linalostahili kupongezwa kwa dhati.

(a) Ni mikakati gani itakayochukuliwa katika kuhakikisha kuwa jengo hilo linaendelea kutunzwa na kuwa katika hali nzuri.

(b) Je, ni kweli kuwa mradi wa ujenzi wa jengo hilo unahusisha pia ujenzi wa nyumba ya Spika pamoja na Hosteli kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu suali la Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini ninaomba kupokea pongezi zilizotolewa na Mhe. Mjumbe. Pongezi zake hizo zinaonesha ni kiasi gani anazithamini juhudi zinazochuliwa na Serikali yetu pamoja na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kuleta maendeleo ndani ya Nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kupokea pongezi hizo naomba sasa kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Katika kuhakikisha kwamba Jengo Jipya la Baraza la Wawakilishi Zanzibar linaendelea kutunzwa na kubaki katika hali nzuri, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi tayari limejiandaa vyema kwa kuimarisha shughuli za matunzo, usafi na matengenezo yanayohitajika ya siku hadi siku. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi imeandaa Watumishi wa kutosha kwa ajili ya kazi hizo. Aidha, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi tayari imeshatangaza nafasi ya kazi kwa ajili ya kupata Msimamizi wa Majengo *"Estate Manager*" ambae pamoja na mambo mengine atawajibika kuishauri Ofisi kitaalamu juu ya matengenezo ya majengo hayo pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa utunzaji wa jengo na vifaa vyake, ambao utaingizwa katika bajeti ya Baraza.

(b) Mradi ya Ujenzi wa Jengo jipya la Baraza la Wawakilishi ni tofauti na Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makaazi rasmi ya

Mhe. Spika, na Mradi wa Ujenzi wa Hosteli ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mradi wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi umetekelezwa kwa msaada wa asilimia 50% kutoka kwa Kampuni ya *Al-Youseif Establishment* inayoongozwa na Sheikh Abdulla Moh'd Al-youseif wa Saudi Arabia na mkopo usio na riba wa asilimia 50% kutoka kwa Jumuiya hiyo ya *Al- Youseif Establishment.*

Kwa mradi wa ujenzi wa Nyumba ya Makaazi rasmi ya Mhe. Spika, unatekelezwa kwa msaada wa fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Fedha zilizopatikana zimewekwa kulipia karibu asilimia 82% ya ujenzi ya nyumba hiyo na asilimia 18% ya fedha zilizobakia italipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa upande wa ujenzi wa Hosteli ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ujenzi huu utakuwa ni mradi mpya ambao ni Awamu ya Pili ya Mradi wa Ujenzi wa Baraza. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi inaendelea na jitihada za kuzungumza na Washirika wa Maendeleo ili waweze kutusaidia katika ujenzi huo. Katika jitihada za kuendeleza mradi huu mnamo mwezi wa Septemba, 2010, Mhe. Spika, na Ujumbe wake walikwenda Nchini Libya kwa ajili ya kufanya mazungumzo yenye lengo la kupata msaada kwa ujenzi wa Hosteli hiyo na tuna matumaini mazuri ya kupata msaada huo kutokana na ziara hiyo. Kwa hiyo napenda nitoe pongezi maalum kwa Mhe. Spika kwa jitihada hizo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba jengo letu no vizuri na nadhani kwa Afrika Mashariki na Kati ni la Mwanzo. Katika wafanyakazi wetu wote tulionao hawana uzoefu wa kuweka usafi katika jengo hili. Tulisikia kuwa kuna Kampuni itapewa tenda hizo. Je, suala hili limeondoshwa na serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Ali Abdulla Ali. Kama nilivyosema awali Mhe. Spika, kwamba jitihada zinachukuliwa na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuhakikisha kwamba Jengo hili linatunzwa na linakuwa safi. Kwa hiyo hatua zote zinazoelekea kutunza jengo hili linatuchukuliwa ikiwemo pamoja na mafunzo kwa wafanyakazi hao ili waweze kufanya hivyo. Kwa sasa hakuna kampuni maalum inayofanya kazi hiyo isipokuwa wafanyakazi wenyewe wa Baraza watakaofanya kazi hiyo.

Mhe. Spika: Unajua masuala yanayomgusa mtu utatamani wakati mwengine usimame mwenyewe, kumbe si utaratibu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri na mimi niungane na wenzangu kukiri kwamba jengo letu ni jengo la kisasa la kifahari ambalo ni jengo ambalo linastahili kutunzwa.

Sasa napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa sababu jengo hili limejengwa na mfadhili na mfadhili tayari ameshatukabidhi. Je, una uhakika wowote ambao kuwa tulipewa endapo jengo hili litakuwa limeharibika litakuwa linafanyiwa matengenezo na mfadhili au ni sisi wenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Kwanza Mhe. Spika, napokea pongezi zake za kupongeza jengo hili. Ni kweli Mhe. Spika, jengo hili ni mfano katika Afrika Mashatiki na hongereni sana kwa kazi hii n zuri.

Mhe. Spika, Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba jengo hili litaendelea kutunzwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na litaendelea kutunzwa kwa hadhii hii hii.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, huku tukisubiri huduma za usafi kwa maana ya watenda kazi. Je, suala la *ECO* Katika ukumbi huu lini litaondoka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa tuna tatizo la *ECO* katika jengo lako hili ningemuomba Mhe. Mwakilishi alirudia suala lake vizuri sikulisikia uzuri.

Mhe. Spika: Tuendelee pamoja na kwa utaratibu upo wa kushughulikia suala la *ECO*. Tunaendelea.

Nam. 19

Uharibifu wa Mazingira kwa Ujjenzi wa Majengo kwenye Fukwe za Bahari

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Hivi sasa kumekuwa na tabia ya wamiliki wa mahoteli hasa ya kitalii kujenga baadhi ya majengo yao juu ya fukwe za bahari kinyume na Sheria za nchi. Kwa kuwa majengo haya hayana mficho; yako dhahiri shahiri.

(a) Je, Mhe. Waziri, Serikali inatoa kauli gani juu ya ujenzi wa aina hii?.

(b) Kuachia ujenzi wa aina hii hapa nchini kwetu kunaashiria nini?.

(c) Je, Mhe. Waziri, kujenga majengo juu ya fukwe za bahari ni uchafuzi wa mazingira au la?.

(d) Je, Idara ya Mazingira itachukua hatua gani ili kukabiliana na jambo hili?.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, Kwa ruhusa na kabla ya kumjibu Mhe. Salmin Awadhi Salmin suali lake Nam. 19 lenye vifungu (a),(b),(c) na (d) naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ujenzi wa majengo ikiwa ni pamoja na hoteli za kitalii na nyumba za kuishi umekuwa ukiendelea kwa kasi katika maeneo yaliyo karibu na fukwe. Hatua hii hufanyika ili kuwawezesha wageni wanaofika kwenye hoteli hizo au familia za wanaoishi katika maeneo hayo ziweze kufurahia mandhari nzuri za bahari ya Zanzibar zikiwemo fukwe. Ujenzi huo hasa wa hoteli za kitalii unadhibitiwa na sheria ya Mazingira ya mwaka 1996 kwa kutaka ujenzi huo ufanyiwe tathmini ya za kimazingira na za kijamii yaani *environmental impact assessment* kabla haujaanza ili kuepusha athari kubwa za kimazingira na kijamiii zinazoweza kutokea kwa kufanyika ujenzi huo.

Mhe. Spika, aidha, ujenzi huo unadhibitiwa na sheria ya Umiliki wa Ardhi nam. 12 ya mwaka 1992 ambayo inaelekeza ujenzi wa mahoteli kwenye maeneo hayo zijengwe umbali wa mita helathini (30) kutoka alama inayofikiwa na maji ya bahari yanapojaa kwa fukwe za mchanga yaani *sand beaches or sea cliff*. Pamoja na kuwepo kwa Sheria hizo bado wapo wawekezaji wachache na baadhi ya wananchi ambao wanakiuka taratibu hizo. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Salmin Awadhi Salmin suala lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, imewataka wawekezaji wanaopatiwa maeneo yaliyo karibu ya fukwe kuyatumia kwa madhumuni waliyoombea na kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo ili kuepuka matatizo ya ujenzi katika maeneo ya fukwe. Aidha, inazitaka taasisi zinazohusika na utoaji wa vibali vya maeneo na ujenzi kufanya hivyo kwa kufuata sheria husika. Kwa wale waliokwishajenga kinyume na taratibu za Kisheria, Ofisi yangu itakaa pamoja na taasisi husika na vyombo vya sheria

ili kulipatia ufumbuzi kwa mujibu wa taratibu na Sheria zilizopo.

(b) Kuachia ujenzi unaokiuka taratibu za kisheria kunaashiria kuwa baadhi ya taasisi husika kutosimamia vyema majukumu yao kunakopelekea kuongezeka kwa uharibifu wa mazingira. Pia kwa wanaofanya hivyo ni sawa na kuidharau serikali inayoongozwa kwa misingi ya Sheria na Utawala Bora jambo ambalo haliwezi kuvumiliwa na Ofisi yangu pamoja na Serikali kwa jumla.

(c) Kujenga majengo juu ya fukwe za bahari si **UCHAFUZI** wa mazingira, bali ni **UHARIBIFU** wa mazingira. Mhe. Spika, **Uchafuzi** wa mazingira kama vile utupaji ovyo taka au kuzagaa kwa mifuko ya plastiki ni tendo linaloweza kurekebishwa kwa gharama ndogo na likafanikiwa kwa muda mfupi ingawa inategemea na ukubwa na uchafuzi uliofanywa; lakini **uharibifu** wa mazingira kama vile mmong'onyoko wa fukwe unaotokana na ujenzi holela fukweni, huu unahitaji gharama kubwa kuweza kufanya marekebisho ya eneo lililoharibiwa na kuna uwezekano mdogo wa kufanikiwa, ama mafanikio yake huchukua muda mrefu.

(d) Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira itaendelea kuielimisha jamii pamoja na wadau wengine ili kukabiliana na tatizo hili. Aidha, itaendelea kushirikiana na taasisi nyengine hasa zinazohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi ili kuhakikisha taratibu za kisheria zinafuatwa kwa ujenzi utakaofanyika kwenye maeneo hayo. Kwa wale ambao watakiuka sheria na taratibu zilizopo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itashirikiana na taasisi husika na vyombo vya Sheria ili kudhibiti matokeo hayo.

Mhe. Salmin Awadhi Salmin: Mhe. Spika, Je, Mhe. Waziri wizara yake imeshafanya tathmini kuona kwamba ni nyumba ngapi ambazo mpaka kipindi hiki zimejengwa kwenye fukwe na ni hoteli ngapi ambazo mpaka sasa hivi zimejengwa kwenye fukwe.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, Ofisi yangu baada ya kupata suala hili imetoa aigiza kwa idara ya Mazingira Kushirikiana na taasisi nyengine za serikali zinazohisika ziweze kufanya tathmini

Juu ya matokeo haya ya ujengwaji wa Fukwe na jinsi gani wa kuweza kushughulikia.

Mhe. Spika: Kuhusu nyumba ngapo nadhani bado tunasubiri hiyo tathmini.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa kuwa dara yake inafanya tathmini ya nyumba ngapi zilizokuwepo kwenye fukwe leo anaweza kutwambia nji *Jet* ngapi
katika Mahoteli zimetolewa kibali na idarayake na zinajengwa hadi sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ofisi
yangu bado haina takwimu hizo lakini namuhakikishia Mhe. Mwakilishi nitamletea taarifa hiyo kwa maandishi. (*Makofi*).

Nam. 75

Wizara mpya zilizoundwa Kutokuwa na Bajeti

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza**:-**

Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa tarehe 31 Oktoba, 2010. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliundwa na Wizara zisizozidi 13 ambapo Baraza la Wawakilishi lililopita katika Mkutano wake wa Ishirini wa Bajeti ya 2010/2011 lilipitisha Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hizo 13 tu. Mara baada ya Uchaguzi Mheshimiwa Rais, kwa uwezo alionao Kikatiba aliunda Serikali yenye Wizara zisizopungua 16.

(a) Kwa kuwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 ilipangwa kwa Wizara 13 tu na kwa kuwa Baraza halikupitisha Bajeti ya Ziada. Je, Wizara zilizoongezeka zitatumia fedha zipi kabla ya kuanza kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

(b) Kwa kuwa hapana utaratibu wa wazi wa Serikali wa kutoa taarifa za mapato, matumizi na bakaa ya fedha kila tunapoingia Awamu mpya ya Uongozi kutoka Awamu ya Zamani. Je, tabia hii haichangii upotevu wa fedha za umma kwa kuweka mianya ya wizi.

(c) Je, Mhe. Waziri ili kuwa na Bejeti ya Ziada (Supplementary Budget) kuna vigezo gani vinavyohitaji kufikiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-
Mhe.Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa, kikatiba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anao uwezo wa kuongeza au kupunguza idadi ya wizara. Kutokana na uwezo huo, mara baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2010, Mhe. Rais aliunda Wizara 16 badala ya 13 zilizokuwepo wakati wa kupitisha Bajeti ya mwaka 2010/2011. Kimsingi, mabadiliko yaliyofanywa na Mhe. Rais, yalilenga zaidi katika kuongeza ufanisi serikalini, ili hatimae wananchi wa Zanzibar waweze kujipatia huduma bora zaidi.

Mhe. Spika, kutokana na maamuzi hayo yaliyofanywa na Mhe. Rais naomba nichukuwe fursa hii mbele ya Baraza lako tukufu kumpongeza sana Mhe. Rais kwa uamuzi wake huo. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo.

(a) Mabadiliko ya idadi ya wizara kutoka 13 hadi 16 yamezingatia zaidi katika kuongeza ufanisi. Hata hivyo, muundo mpya wa wizara 16 umetokana na wizara zile zile 13, kwa baadhi ya Idara kuziundia Wizara (mfano Mifugo na Uvuvi, Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na vile vile kuziondoa baadhi ya Idara katika wizara nyengine (mfano Ustawi wa Jamii)

Mhe. Spika, mabadiliko hayo, kwa wakati huu hayajahitajia bajeti ya ziada. Kilichofanyika ni kuanzisha mafungu mapya kwa wizara mpya. Idara na Taasisi zinazounda wizara zinahama au kuhamia na bajeti yake kama ilivyoidhinishwa awali na Baraza hili tukufu. Aidha hatua zimechukuliwa za kugawanya bajeti iliyoidhinishwa kwa Idara ya Mipango zihudumie wizara hizo mpya. Kwa kutambua pia uwezekano wa kutokea mabadiliko ya muundo wa Serikali, Bajeti ya mwaka 2010/11 ilikuwa na kasma maalum ya marekebisho ya mshahara chini ya Wizara ya Fedha na Wchumi. Kasma hii imetumika kwa ajili ya mishahara ya Viongozi wa Wizara mpya ambao hawakuwepo kulingana na muundo wa Wizara 13. Kwa ujumla, marekebisho haya yamezingatia Mamlaka ya Waziri inayosimamia fedha, ya kuweza kuhaulisha huwa haupelekei jumla ya Bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kubadilika.

(b) Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Fedha za Umma zinaitaka Serikali kuwa wazi na kuwajibika katika fedha za Umma. Kwa msingi huo, hesabu za Serikali hukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, Kamati za Baraza *PAC* na ile ya Fedha na Uchumi hupatiwa taarifa za hesabu za Serikali na hatimae, hesabu hizo huwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu. Hatua hii inadhihirisha kuwa Serikali inao utaratibu wa wazi wa kutoa taarifa za mapato na matumizi.

Mhe. Spika, kwa kuwa utaratibu wetu wa Uchaguzi Mkuu ni kuwa na uchaguzi kila baada ya Miaka Mitano na katika mwezi wa Oktoba, wakati Bajeti huanza Julai, na kuishia Juni mwaka unaofuata. Hivyo, awamu inayoondoka madarakani hupata miezi 4 ya kuendesha bajeti na ile anayoingia madarakani hupata miezi 8 ya bajeti. Kwa utaratibu huo, awamu inayoondoka hutayarisha na kukabidhi taarifa ya kukabidhi Ofisi kwa awamu inyoingia madarakani. Taarifa hiyo hujumuisha pia hali ya fedha. Utaratibu huu wa makabidhiano ni mzuri na hauchangii upotevu wa fedha za Umma, kwa kiongozi anaeingia madarakani atakuwa anaelewa fedha zilizopo.

(c) Mhe. Spika, kifungu Nam. 17 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2005, kinaelekeza kwa ufasaha vigezo vinavyotakiwa kufikiwa ili kuwe na bajeti ya ziada yaani *Supplementary Budget*. Vigezo hivyo ni kama ifuatavyo:-

- Kuwepo kwa mahitaji ya ziada na yawe ya lazima ambayo hayakuonekana wakati wa uwasilishaji wa Bajeti, yatakayozidi jumla ya kiwango cha matumizi kilichoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

- Kuwepo na uwezekano wa kukusanya mapato kwa kiwango hicho cha ziara kinachohitajika.

Mhe. Hija Hassan Hija:

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba serikali imeenda katika mpango mpya lakini haikuathirika na kwa kuwa taaluma hii ni kubwa na inahitaji Wajumbe kuijua. Je, yuko tayari sasa Wajumbe wake

kuwafundisha angalau mpango mzima wa serikali mpya ili tukawa na uelewa katika jambo hili.

(b) Kwa kuwa Kamati ya Fedha na *PAC* amekiri kwamba zina jukumu la kusimamia mipango na m atumizi mazuri ya fedha za Umma atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya Kamati ya Fedha saa zote hata zile zile zenye mipango ya uchumi wa nchi badala ya kupewa Wizara ya Biashara na Wizara ya Fedha na Kilimo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, hapa juu pana matatizo makubwa sana kwa sababu ya *echo* maswali yake yote mawili sikuyasikia.

Mhe. Spika: Mhe. Hija rudia kwa utulivu na utaratibu sana ili waziri aweze kufahamu.

Mhe. Hija Hassan Hija:

(a) Mhe. Spika, taaluma ambayo Mhe. Waziri ameitoa juu ya suala zima la muundo wa Serikali na bajeti ya ziada ni taaluma muhimu sana kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Je, yupo tayari kutupatia mafunzo juu ya uelewa wa jambo hili ili tukawa na uelewa nalo.

(b) Kwa kuwa Kamati ya Fedha na *PAC* ni muhimu sana kwa usimamizi wa mali ya serikali na uchumi. Atakubaliana na mimi kwamba Kamati ya Fedha kuna haja ya kukagua wizara zote hata zile zenye mipango ya maendeleo kama Wizara ya Uvuvi na Mifugo, badala ya kubakia Kamati ile kukagua Wizara ya Fedha, Kilimo na Biashara peke yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kuna haja ya kulifanyia marekebisho hili Baraza kwa sababu *echo* iliyopo kwa sababu ukikaa juu huwezi ukasikia.

Lakini naomba nijibu maswali mawili ya Mhe. Hija kama nimeyafahamu vizuri kama ifuatavyo.

(a) Wizara yangu haina matatizo katika kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa katika maeneo ya bajeti ya ziada.

Sisi tunaamini kama Wizara kama Serikali tukitoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wakatufahamu vizuri wataweza kusaidiana na serikali yao.

(b) Kama nimemfahamu vizuri Mhe. Mwakilishi anataka Kamati hizi za Fedha na Kamati ya *PAC* ikague taasisi zote za uchumi badala ya kuachiwa Kamati nyengine.

Mhe. Spika, mimi kama Waziri ambaye nasimamia sekta ya fedha na mipango na uchumi sina tatizo na hilo, lakini yapo katika mamlaka ya Mhe. Spika na Baraza lenyewe.
Kamati ya Fedha na Kamati ya *PAC* ikipewa dhamana hiyo na Baraza hili mimi naamini watafanya kazi hiyo na sisi Wizara ya Fedha hatuna matatizo kabisa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimuulize swali la nyongeza rafiki yangu Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Katika majibu yake amegusia suala la mianya ya wizi na matumizi mabaya ya fedha za umma upotevu wake, yanashughulikiwa kutokana na kuwepo ukaguzi kupitia Afisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Jana Mhe. Spika, tumesoma gazeti la Zanzibar Leo nikanukuu mkutano wa Mhe. Waziri na Wahasibu wa Wizara mbali mbali wakilalamikia kwamba Makatibu Wakuu wa Wizara ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wamekuwa chanzo kikubwa cha matumizi mabaya na upovu wa fedha. Nasoma kama ilivyoandikwa kwenye gazeti kutokana na kutoshughulikiwa ripoti na mapendekezo ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Waziri anaweza kutusaidia kwamba Wizara yake ina mpango gani kwa sababu ndio yenye dhamana ya kusimamia hili kwa ujumla wake kuona Makatibu Wakuu wa Wizara zote wanatekeleza mapendekezo yale na wanaifanyia kazi ripoti ya Mkaguzi Mkuu ili upotevu wa fedha za wananchi walipa kodi usiendelee katika nchi yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kweli nimefanya mkutano na Wahasibu Wakuu wa Serikali pamoja na wakaguzi wa ndani na ni kweli kwamba wakaguzi walilalamika kwamba ripoti wanazozitoa mara nyingi huwa hazisomwi na Makatibu Wakuu.

Sisi kama Wizara tumechukua hatua mbili ni kama hizi zifuatazo:

Hatua ya kwanza nimemuomba Katibu wangu Mkuu andae waraka, ayaainishe baadhi ya matatizo yaliyokuwepo ndani ya ripoti za wakaguzi wa ndani ili afanye *presentation* kwa kikao na Makatibu Wakuu ili kuweza kuona kwamba haya ni maeneo ambayo yanapaswa kushughulikiwa ndani ya Wizara zetu zote.

Hatua ya pili nimemuomba Mhe. Rais, nitawasilisha waraka ambao utakaoeleza taratibu zote na mambo yote yaliyojitokeza katika kikao cha Baraza la Mawaziri ili na mawaziri na wao waweze kuyaelewa na waweze kufanya kazi kwa karibu zaidi na Makatibu Wakuu.

Ripoti za wakaguzi wa ndani zinaumuhimu mkubwa sana. Kupitia kikao chako Mhe. Spika, nawaomba sana Makatibu Wakuu wawe wanazisoma.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Ukiachia mbali mawaziri ambao wametengewa fungu katika bajeti iliyopita. Tutakumbuka kuwa serikali mpya imemuingiza madarakani kiongozi mwengine Makamo wa Kwanza wa Rais ambaye huyu ana bajeti kubwa kwa mujibu wa matumizi ya Afisi yake.

Je, kiongozi huyu anatumia fungu gani na kwa kuwa bajeti yake ni kubwa katika matumizi ya afisi yake na kwa kuwa kipindi kilichobakia ni nusu ya mwaka wa bajeti yaani miezi sita (6). Je, fungu lililopo lina uwezo wa kukidhi bajeti ya kiongozi huyu pamoja na mawaziri wengine.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nieleze kwamba katika awamu ya sita (6) kulikuwa kuna Mhe. Rais, Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na kulikuwa kuna bajeti za taasisi hizi tatu.

Katika awamu hii ya saba (7) kuna Mhe. Rais, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais. Tukiseme ki-*level* tuko katika *level* tatu. Tulichokifanya kwenye *level* hizi tatu, tumeangalia ile bajeti ambayo iliyokuwepo kwa Mhe. Waziri Kiongozi, tumeangalia bajeti iliyokuwepo kwa Naibu Waziri Kiongozi. Tukaangalia majukumu ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, tukaangalia kinachohitajika kuongezwa katika fedha zetu tulizonazo zile nilizosema zipo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, tumejaribu kuongeza *portion* huku na kuongeza *portion* huku.

Ninaimani kwamba fedha zilizopo Waheshimiwa Makamo wetu wawili hawa zitawatosha na kama hazikuwatosha basi tutaweza kumshauri Mhe. Rais ili kuweza kutafuta fedha za ziada ili tuweze kuomba *supplimentary budget*. Ninaimani kwamba zitawatosha.

Nam. 23

Kuongezwa kwa Maslahi ya Wafanyakazi

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza**:-**

Mhe. Spika, moja ya ahadi ya Mhe**.** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika mikutano yake ya Kampeni ni kuangalia maslahi ya watumishi wa umma.
Kwa kuwa kima cha chini cha mishahara kwa watumishi wa umma ni shilingi laki moja (100,000/=) kwa mwezi, na kwa kuwa kiwango cha mishahara kwa watumishi kama hawa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni shilingi laki mbili na sitini elfu (260,000/=) kwa mwezi.

Je, Mhe. Waziri, Serikali ina mipango gani ili kuona kwamba maslahi ya watumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanafanana, hasa ikizingatiwa kwamba soko letu la biashara na sarafu yetu ni moja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza Mapinduzi wa awamu wa saba Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein katika mikutano yake mbali mbali ya kampeni aliahidi kunyanyua maslahi ya watumishi wa umma. Hatua ya awali aliyoichukua Mhe. Rais ya kulishughulikia suala la wafanyakazi ni kuunda wizara maalum iliyo chini ya afisi yake itakayosimamia utumishi wa umma na utawala bora ili taratibu za watumishi na maslahi yao yaweze kuangaliwa kwa umakini zaidi.

Mhe. Spika, maslahi ya wafanyakazi yana nyanja pana yanahusisha mishahara na nyanja zake, muundo wa utumishi, kupandishwa vyeo, mafunzo, mafao ya kustaafu, sheria bora za kazi na kadhalika. Katika kuyasimamia haya ni lazima kuwe na uwiano mzuri kati ya hali ya uchumi na marekebisho ya maslahi, ikizingatiwa kuwa malipo ya mshahara ni kitu cha kudumu katika malipo ya serikali na yanapaswa kulipwa kwa wakati na kila mwezi bila ya kukosa.

Si vyema kuwa na mshahara ambao hauna uhakika wa kulipika kila mwezi. Katika upangaji wa mishahara kila nchi au serikali duniani hupanga kima cha chini na muundo wa mishahara kwa mujibu wa uwezo iliyonao hata kama wanatumia sarafu moja kama nchi nyengine, kwa mfano za Ulaya zinatumia sarafu moja za Euro na masoko yao yanafanana lakini mishahara yao kwa kuzingatia sababu hizo za kiuchumi ndizo zilizopelekea Zanzibar na Tanzania Bara kutofautiana kwenye kima cha chini cha mishahara ambapo Zanzibar kima cha chini ni shilingi laki moja na Tanzania Bara ni shilingi laki moja la thalathini na tano na sio laki mbili na sitini kama anavyodai Mhe, Mwakilishi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Serikali kila inapopanga kima cha chini cha mshahara huwa inazingatia kiasi kinacholipwa kwa watumishi wa Serikali ya Muungano. Huwa mara zote inapanga kiwango ambacho hakitofautiani sana ingawaje uchumi wetu ni mdogo ukilinganisha na ule wa Tanzania Bara. Lengo la Serikali iwapo uchumi utaruhusu kuweka maslahi bora zaidi ya wafanyakazi wake na ikiwezekana hata zaidi ya yanayotolewa na Serikali ya Muungano.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na maelezo mazuri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ninavyoelewa mimi na kwa mujibu wa matangazo kima cha chini cha mshahara katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni shilingi laki mbili na sitini. Kwa kuwa Serikali zetu zote mbili zinaendeshwa kwa misingi ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na kwa mujibu wa Katiba zetu zote mbili.

Na kwa kuwa msingi mkuu wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ni kuona watumishi wa Umma hasa katika daraja zinafanana ni kwamba mishahara yao haipishani pakubwa. Na kwa kuwa sasa hivi kuna mapishano makubwa ya kimaslahi katika mishahara katika serikali zetu zote mbili. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba ikiendelea kuwa na mapishano makubwa ya kimaslahi kwa kiasi kikubwa kama hicho kunakiuka misingi ile ya siasa ya ujamaa na kujitegemea.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kabla sijajibu swali la msingi nitoe ufafanuzi juu ya suala zima la utafiti tuliofanya kuhusu kima cha chini cha mshahara wa Tanzania Bara unaolipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Na nilikiri kwamba sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunapotaka kupanga kima cha chini cha mshahara mara nyingi sana huwa tunazingatia kima cha

chini ambacho kinalipwa na wenzetu. Wakati mwengine Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa inakitangulia hicho kima cha chini cha mshahara cha Tanzania Bara.

Ninachotaka kusema kwamba baada ya utafiti wetu kima cha chini cha mshahara kinacholipwa sasa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kutoka laki moja na thalathini na tano elfu (Shs 135,000/=) mpaka laki moja na thamanini na tisa elfu (Shs 189,000/=).

Tafsiri ya kima cha chini cha mshahara inategemea na muda wa mtu ambao anayeanza kazi sasa na yule ambaye analipwa kima cha chini cha mshahara ambaye amefanya kazi kwa muda mrefu kufuatana na majukumu, uwezo na nafasi anayoifanyia kazi. Tunachotaka kusema kwamba sisi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tutajitahidi sana tusivuke misingi hiyo ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Ndio maana nilisema kwamba pale kwa maana ya kuweka usawa kwa wananchi wetu kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Pale mwanzo nilisema kwamba hivi sasa Mhe. Rais ameiunda hii Wizara kwa lengo hilo. Kwa hivyo namuomba Mhe. Mwakilishi atusubiri kidogo na kwa sababu hii Wizara imeundwa na kwa sababu Mswada wa Sheria unakuja unaoweza kuzingatia hayo, basi ni vizuri Mheshimiwa aridhike na hili ninalolisema. Hiyo ndio hali halisi ilivyo, ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya ya Mhe. Waziri wa Utumishi na Utawala Bora naomba kuongezea kidogo ili Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali lake apate upeo mzuri wa kufahamu.

Kwanza nataka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba mimi nilikuwa ni Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kima cha chini cha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakijafika shilingi laki mbili na sitini.

Lakini pia nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi katika kupanga mishahara hatuangalii tu hali ya uchumi na mapato ya nchi, vile vile tunaangalia wastani uliopo baina ya watumishi waliokuwemo ndani ya Serikali, *visa versa* idadi ya watu iliyopo.

Tanzania Bara sasa hivi watumishi wote waliyokuwepo ndani ya Serikali ni asilimia 9 ya *population* yao, lakini watumishi waliyokuweno ndani ya Serikali ya Zanzibar ni asilimia 28 ya idadi ya watu wa Zanzibar. Hii inadhihirisha wazi kwamba sekta binafsi kwa upande wa Zanzibar bado ni changa. Watu wetu wengi wanakimbilia kuajiriwa ndani ya Serikali. Nitaziomba sana sekta binafsi

kuandaa mazingira ya kuwaajiri Wazanzibari ili serikali iweze kuwaajiri Wazanzibari wachache zaidi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Waheshimiwa Mawaziri naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mbali ya kutumia kigezo cha kuangalia kima cha chini cha mshahara wa kutoka Tanzania Bara na kwengine. Kuna utafiti uliofanywa wa matumizi ya kaya ambayo yale ndio uhalisia wa matumizi ya mtu wa kawaida. Kwa nini Serikali haitumii kigezo hiki kwa kuangalia ripoti ya matumizi ya kaya kuwa ndio kigezo au ndio msingi wa kupanga bajeti kwa watumishi wetu wa umma.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, utafiti ndicho kigezo ambacho huwa kinatumiwa katika masuala mengi ya uendeshaji wa serikali na hasa utafiti huo ukiwa umeshapelekwa katika Tume ya Mipango ya nchi. Napenda kumuhakikishia kwamba utafiti huo utaendelea kutumika lakini pia utategemea na hali halisi ya uchumi wa nchi ilivyo kama nilivyosema hapo awali.

Nam. 54

Serikali Kuzisaidia Jumuiya za Kiraia:

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza**:-**

Jumuiya za kiraia zina mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya Zanzibar; kwa kuwa Jumuiya hizo zinategemea misaada kutoka kwa Wafadhili hususan nje ya Zanzibar.

(a) Je, Mhe. Waziri Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuzisaidia Jumuiya hizo kifedha hata tukizingatia kuwa zina mchango mkubwa katika kujenga taifa.

(b) Serikali haioni kuwa ipo haja ya kupatiwa Mwakilishi wao katika Baraza la Wawakilishi ambaye pamoja na mambo mengine, atafuatilia kwa karibu zaidi masuala ya Jumuiya za kiraia.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 54 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Jumuiya za Kiraia zina mchango mkubwa sana kwa Maendeleo ya Zanzibar.

(a) Mhe. Spika, ni kweli ipo haja kwa Jumuiya hizo za Kiraia hapa Zanzibar kusaidiwa kifedha na serikali kulingana na mchango wake katika jamii yetu. Hata hivyo, hizi ni Jumuiya za hiari, ni jumuiya za kujitolea. Dhana hii ya msingi ya Jumuiya hizi za hiari yaani kujitolea kwa hali na mali huwa inafahamika na Wanajumuiya wote tokea katika hatua za uanzishwaji wake.

Jumuiya hizi huwa ni Jumuiya za watu wa kundi maalum la wanajamii ambao baada ya kukerwa au kuguswa na tatizo fulani katika jamii, na baada ya kujipima, wakaona kwamba ama kwa kutumia utaalamu walionao au kwa kutumia rasilimali walizonazo au kwa kutumia uwezo walionao wa kuweza kukusanya rasilimali zinazohitajika, wanao uwezo wa kusaidia kutatua tatizo hilo lililoko katika jamii hiyo. Jamii hiyo huungana pamoja na kuanzisha Jumuiya yao kwa lengo la kufanikisha malengo yao hayo.

Moja kati ya yanayowasukumu wanajumuiya hufanya haya ni kule kuelewa kwamba ingawa ni serikali yenye wajibu wa kuyatatua matatizo hayo, lakini yenyewe haina uwezo wa kutosha wa kuyakabili na kuyamaliza matatizo hayo. Ndio maana na wao wakapata moyo wa kutaka kusaidia katika msingi huu. Msaada wa kifedha wa serikali kwa Jumuiya hizi utategemea zaidi hali ya kifedha iliyonayo serikali. Bila ya shaka sote tunaelewa hali mbaya ya kifedha inayoikabili serikali hivi sasa.

Hata hivyo, serikali imekuwa ikizisaidia sana Jumuiya za Kiraia kwa njia mbali mbali kama vile kuzitambua, kuzishirikisha katika kupanga mipango ya maendeleo ya Kitaifa na kuzipa misamaha ya kodi yenye thamani ya mamilioni ya shilingi. Huu ni msaada na mchango mkubwa sana kwa serikali yetu kwa taasisi hizi za kiraia.

Hata hivyo, Mhe. Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba Asasi hizi za kiraia hapa Zanzibar bado kabisa hazijaonesha wala hazijajipanga vizuri katika kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa uwazi kwani hazijawajibika katika kutekeleza majukumu yao ya kisheria kama vile kuwasilisha ripoti za utendaji kazi zao kwa kila mwaka.

Aidha Jumuiya nyingi, hata zile zinazoonekana kwa macho kufanya vizuri, zimeshindwa kuwasilisha ripoti za ukaguzi wa mipango na matumizi ya fedha ikiwa ni pamoja na fedha nyingi wanazopokea

kutoka kwa wafadhili. Sasa ni azma ya Wizara yangu kuwa na kitengo maalum cha kufuatilia hayo.

(b) Kuhusu suala la Jumuiya za kiraia kupatiwa nafasi maalum za Uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi linaonekana zaidi ni suala la kisera na la kisiasa.

Kisiasa ni kwa maana kuwa ni suala litakalohitajika mjadala wa kisiasa utakaopelekea kuandaliwa kwa mapendekezo ya marekebisho ya Katiba ya Zanzibar yatakayoingizwa na kutambua kuweko kwa nafasi hizo maalum. Ugumu wa hili ni uwezekano wa kuzusha mjadala wa makundi mengine ya watu walio katika mazingira magumu kama vile vijana, walemavu na makundi mengine muhimu yanayosaidia jamii yetu kwa ujumla, pia kutaka na wao kuingizwa na kutambuliwa katika Katiba.

Kisera kwa maana ni maamuzi ya kufanywa na vyama vya siasa vyenyewe kwa kutenga nafasi maalum kwa ajili ya uwakilishi wa aina hiyo kupitia nafasi za viti maalum kama vinavyofanya baadhi ya vyama hivi sasa kwa kutenga nafasi za Uwakilishi kwa makundi maalum yaliyo katika mazingira magumu; au kupitia nafasi zao za viti maalum vya kugombania katika vyama vyenyewe ili kutoa uwiano sawa kwa wanachama ndani ya Vyama vyenyewe, kama ilivyo nafasi nyengine za walemavu, vijana na wanawake.

Mhe. Ismail Jusa Ladhu: Mhe. Spika, kwa sababu Waziri katika majibu yake amegusia suala la kutumia vibaya hususan kuanzishwa jumuia za kiraia. Na kwa sababu tunaelewa kwamba zipo jumuia nyingi ambazo zinaitwa *Briefcase* ya *NGO's* ambazo zipo katika mikoba ya walizozianzisha, isipotambulikana kuwepo kwa Ofisi wala kazi maalum zinazoeleweka. Kuwepo kwa jumuiya kama hizi kumekuwa kukitumiwa vibaya fursa zinazotolewa na wafadhili kusaidia maendeleo. Je, wizara yake haioni kuna haja sasa kufanya tathmini ya kuzitambua jumuiya kama hizo na kuzichukulia hatua ikiwemo kuzifuta ili kutoa fursa kwa wengine watakaoazisha jumuiya makini za kutoa huduma kama hizo ziweze kusajiliwa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, katika jibu langu mama nilisema kwamba hivi sasa adhma ya wizara yetu ni kuwa na kitengo maalum cha kufuatilia mambo kama hayo, na kitengo hiki hivi sasa tumeshakiunda na shughuli hizo ambazo kitengo hiki tumewapa ni pamoja na kufuatilia utendaji halisi wa jumuiya hizo.

Mhe. Spika, kama zimekidhi haja kwa mujibu wa katiba na sheria basi jumuiya hizo zitaendelea na kama zimekwenda kinyume na utaratibu ambao umewekwa katika usajili wao basi jumuiya hizo tutazifuta.

Nam. 33

Utaratibu wa Utoaji wa Bidhaa kwenye Makontena

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Shirika la Bandari la Zanzibar linawajibu wa kuwahudumia wananchi wake wanaohitaji huduma mbali mbali za kibandari iwe wasafiri au wafanyabiashara. Kwakuwa sasa hivi kumekuwa na huduma nzuri sana kwa wanaosafiri nje ya Zanzibar. Hatahivyo, kumekuwa na manunguniko miongoni mwa wafanyabiashara juu ya utaratibu unaotumika hususan wakati wa utoaji wa bidhaa kwenye makontena.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwani utaratibu upi hutumika ili wafanyabiashara waweze kutoa bidhaa zao ndani ya makontena yao.

(b) Je, Mhe. Waziri, wizara yako itahakikisha vipi kuwa manung'uniko haya yanapungua au kuondoka kabisa.

(c) Mhe. Waziri ile ahadi ya kujenga jengo maalum kwa ajili ya viongozi mashuhuri (*VIP LOUNGE*) katika bandari ya Zanzibar pale wanaposafiri umefikia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, utaratibu wa kutoa mizigo ndani ya makontena, kwanza mfanyabiashara kuwa na hati ya kutolea mizigo hiyo (*bill of landing*) ambayo tayari ishapigwa mihuri ya Shirika la Meli na Bandari baada ya kufanya malipo husika, pia apate ruhusa ya Mamlaka ya Bodi ya Mapato – *TRA* (*Release Order*) ndiyo aandikiwe *"Gate Pass"* ya kutolea mzigo.

Baada ya hapo mfanyabiashara anawajibika kuwasilisha nyaraka zote kwa Shirika la Bandari na mwisho huruhusiwa kukata nakiri (*seal*) ya kontena akiwemo Ofisa wa *TRA* na baada ya hapo mfanyabiashara huandikiwa risiti ya kutolea mizigo bandarini ambayo husainiwa na mfanyabiashara mwenyewe.

(b) Mhe. Spika, manung'uniko hutokea kwa sababu kuna ufinyu mkubwa wa nafasi bandarini na hali hiyo baadhi ya wakati inasababisha makontena kupangwa manne (4) kwenda juu. Tatizo linalojitokeza ni pale ambapo mfanyabiashara anapoomba kutolewa kontena lake liliopo katikati ya makontena yaliyopangwa …

Mhe. Spika: Mheshimiwa umejibu maswali ya msingi ambayo ilikuwa ni (a) na (b) sijui umeyamaliza yote.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ndio nimeyamaliza yote.

Mhe. Ismail Jusa Ladhu: Mhe. Spika, nashukuru kwa mara nyengine tena kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni kwamba hivi sasa kumekuwa na ushindani mkubwa katika Bandari za Afrika Mashariki katika kuvutia biashara hasa hii ya kuteremsha mizigo katika bandari zake. Mhe. Spika, kwa kuzingatia katika Tanzania hii eneo la Dar es Salaam linaonekana kuzidiwa na nchi jirani kuonekana kujaribu kuvutia fursa hizi.

Je, wizara haioni kwamba kuna haja ya kuimarisha huduma za upakuzi wa mizigo na hasa kutoka katika makontena ya bandarini ili kuvutia wafanyabiashara wengi kuteremsha mizigo yao Zanzibar na kuiongezea mapato Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli bandari yetu imekuwa ina matatizo ya kuchukua muda wa utaratibu wa kushusha makontena, lakini kuchelewa kwake ni kuwa kunatokana na sababu nyingi zikiwemo ufinyu wa eneo husika la kuweza kupanga makontena. Aidha, namuomba Mhe. Mwakilishi kuwasaidia wafanyabiashara wetu ili waweze kutoa makontena yao kwa muda mfupi ili kuweza kutoa nafasi ya makontena kwenye meli zinazokuja hapa Zanzibar na kupata nafasi ya kuweka makontena hayo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi nyengine yakuongeza maelezo zaidi juu ya majibu ambayo Mhe. Naibu Waziri amekuwa akiyatoa.

Mhe. Spika, pamoja na matatizo ambayo tunayo katika bandari yetu, lakini bandari yetu imepata sifa ukilinganisha na bandari ya Dar es Salaam kwa uwezo wa kutoa makontena au mizigo yote kuteremsha kwenye meli na hata kupakia. Mhe. Spika, kazi inayofanywa Dar es Salaam siku tatu basi hapa inafanywa siku moja. Kwa hivyo, hatua ambazo tunaendelea nazo kuboresha hilo tumeagiza vifaa vinavyohusika kwa ajili ya kurahisisha zaidi kazi za kuteremsha na kupakia mizigo.

Mhe. Spika, hilo nina hakika kwamba litazidi kuwavutia wafanyabiashara ambao wakiweko Dar es Salaam wanachukua muda mrefu, lakini wakiwepo hapa wanachukua muda mfupi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo pia naomba niongeze katika Bandari ya Zanzibar sasa hivi kumerundikana makontena mengi, makontena ambayo sababu kubwa ni wafanyabiashara wenyewe.

Mhe. Spika, bandari yetu ni ndogo ukilinganisha na shughuli zilivyo, na kwa hivyo tunatoa wito kwa wafanyabiashara wote wanaoleta mizigo yao kwa kupitia Bandari ya Zanzibar kuhakikisha wamefanya *clearance* ya mizigo yao. Mheshimiwa hii inawezekana mapema kabisa kabla hata meli haijafika na kwa kuzingatia hayo tumeweza kufanya utaratibu wa kuweka vivutio.
Mhe. Spika, k.ama mfanyabiashara yeyote kuanzia tarehe 01/01/2011 atakuwa tayari kutoa mzigo wake baada ya kufanya *clearance* ya kulipa kodi na mambo mengine yote wakati meli iko pale inateremsha makontena. Kwa hivyo, tunasamehe gharama za upakiaji wa kontena kwenye gari lake ya shilingi 50,000/= kwa kontena la futi 20 na shilingi 80,000/= kwa kontena la futi 40. Hizo ni gharama ambazo kama mfanyabiashara yuko tayari kuchukua mzigo wake mara unapoteremshwa kwenye meli na kumpakilia kwenye chombo chake basi gharama hizo tumefuta, vyenginevyo gharama hizi zitaendelea.

Mhe. Spika, kama hiyo haitoshi Shirika la Bandari katika mwezi wa Februari mwaka huu limeandaa *forum* maalum ya siku moja ya wafanyabiashara wote kukaa pamoja na kubadilishana mawazo. Moja ya ajenda ikiwa ni namna bora ya wafanyabiashara kuondokana na matatizo yaliyoikabili bandari kwa sababu ya wao. Mhe. Spika, katika *forum* hiyo baadhi ya wajumbe wako walikuwemo kwenye Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi nao wataalikwa.

Mhe. Spika, hivi sasa katika Bandari ya Zanzibar kuna makontena ya bidhaa yamekaa pale zaidi ya miezi sita. Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria iliyounda shirika hili *Act No.1* ya mwaka 1997 kifungu 42 (2c) kinaipa haki Shirika la Bandari kuzipiga mnada bidhaa zote ambazo ziko pale kwa zaidi ya miezi mitatu na kuna bidhaa zina zaidi ya miezi sita. Kwa hiyo, naliagiza shirika kwa kupitia Baraza hili wawape *notice* wafanyabiashara wote ambao hadi sasa hawajachukua mizigo yao imekaa pale kwa zaidi ya miezi sita, wawape *notice* ya mwezi mmoja vyenginevyo sheria hii tutaitumia kwa kuziuza bidhaa.

Mhe. Spika, tunafanya hivi ili kuhamasisha kwa sababu manung'uniko yamekuwa mengi, makontena yaliyoko pale miezi sita kila mtu ana sababu, wengine meli zinafika mtu hana *bill of landing*. Kwa hivyo, hatuwezi kutoa kontena kwa sababu mtu tu amekuja ni kontena lake, hivyo basi tunatoa wito wafanyabiashara watusaidie katika hili kwani serikali ina madhumuni

makubwa kabisa mazuri kwa sababu bandari ndio uti wa mgongo wa uchumi huu. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumsaidia Mhe. Naibu Waziri wangu.

Nam. 39

Ujenzi wa Barabara za Ziwani na Wete

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Pamoja na kwamba juhudi za ujenzi wa barabara kuu na zile za mitaani (*feeder roads*) zikiimarika Zanzibar kwa muda mrefu sasa kuna maeneo mengine ikiwa ni pamoja na Jimbo la Ziwani, ujenzi huu wa barabara haujatekelezwa ipasavyo.

(a) Mhe. Waziri unaweza kukubaliana na mimi kwamba njia sita za *'feeder roads'* zilizomo katika Jimbo la Ziwani hazijashughulikiwa mpaka sasa.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuhakikisha kwamba ujenzi wa njia hizo unamalizika.

(c) Kwa kuwa wizara imekuwa ikitoa maelezo ya kutatanisha na jawabu zisizoeleweka kuhusu ujenzi wa barabara ya Wete-Chake kupitia Ziwani. Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba umefika wakati, wizara kutoa jawabu sahihi kuhusu kuwemo kwa barabara hii katika orodha ya miradi

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-
Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 39 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali mama naomba kutoa ufafanuzi juu ya majukumu ya ujenzi na utunzaji wa barabara katika visiwa vyetu kwa maana ya kwamba Unguja na Pemba. Mhe. Spika, ni kwamba barabara zetu zimegawika katika mafungu matatu makuu, mafungu hayo ni kama ifuatavyo.

1. Barabara kuu
2. Barabara zinazounda barabara kuu na
3. Barabara ya ndani zinazoingia katikati ya miji ama vijiji.

Pia naomba kueleza kuwa sio kila barabara ama njia inayounda barabara kuu inaweza kuitwa *main road* au *feeder road* bali mgawanyo huo wa barabara hizo ni zile zilizoanishwa ndani ya sheria ya barabara.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa mgawanyo huo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina jukumu la kushughulikia makundi mawili ya kwanza kwa

maana ya kwamba barabara za *main road* na zile za *feeder road*, barabara za ndani zilizomo katika miji ni jukumu la Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, swali la Mhe. Mwakilishi linahusisha barabara zilizo katika kundi la tatu ambazo ni zile barabara zilizokuwa hazimo katika majukumu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano chini ya usimamizi wa wizara hii.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa wizara yangu haina jukumu la moja kwa moja kushughulikia barabara kama suala la Mhe. Mwakilishi ninavyolieleza. Lakini kwa kuwa serikali ina jukumu la kutoa huduma kwa wananchi, basi wizara yangu imekuwa ikishughulikia barabara hizo na mara nyingi kushirikiana na mamlaka husika na pia watu binafsi katika kuondoa matatizo yanayowakabili.
Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba barabara kadhaa katika jimbo lake ziko katika hali mbaya hasa baada ya vipindi vya mvua na pia ni kutokana na kwamba barabara hizo sio za lami, hali ambayo husababisha kutokea maharibiko ya mara kwa mara. Aidha, tumekuwa tukishughulikia barabara hizo kila hali inapokuwa inaruhusu na kuwa na mashirikiano na wananchi wa jimbo hilo.

Mhe. Spika, barabara ya Wesha hadi Mkumbuu hivi sasa imo katika matengenezo na imekamilika barabara yote. Pia barabara ya Kwale hadi Kidemeni yenye urefu wa kilomita 1.5 imefanyiwa matengenezo miezi miwili iliyopita kushirikiana na nguvu za wananchi wa eneo husika. Barabara ya Gombani hadi Michugwani yenye urefu wa kilomita 2 imefanyiwa matengenezo kipindi cha nyuma na hali yake sio mbaya sana. Hivyo, kwa kushirikiana na wananchi barabara hiyo ilipangiwa mawe kwa namna inavyofanyiwa ukarabati.

Mhe. Spika, vile vile barabara ya Mchangawakwale hadi Pembeni yenye urefu wa kilomita 2.5 imepangwa kushughulikiwa katika robo hii ya mwaka wa fedha. Pia barabara ya Mchangawakwale hadi Kichuuwani yenye urefu wa kilomita 4 tumeingiza katika mpango wa kufanyiwa matengenezo katika mwaka ujao wa fedha kwa kutumia fedha kutoka mfuko wa barabara na barabara ya Ziwani hadi Mbuzini yenye urefu wa kilomita 4 bado hatujaipangia ila tunaomba Mhe. Mwakilishi awasiliane na sisi ili tuweze kuunganisha nguvu zetu kwa pamoja kutatua tatizo la ubovu wa barabara hii.

Pia barabara ya Kijangwani hadi Birikau yenye urefu wa kilomita 3 ilijengwa kwa kutumia urefu wa kilomita 1 ya mwanzo na kilomita 2 zilizobakia tumeshazifanyia *grading* hivi karibuni, hivi sasa tunasubiri marekebisho katika

eneo la kwanza yakamilike ili tuweke kifusi katika maeneo mabaya ya barabara hiyo.

Mhe. Spika, napenda kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba wizara yangu haijawahi kutoa maelezo ya kutatanisha na jawabu zisizoeleweka kuhusu ujenzi wa barabara ya Wete kwenda Chake chake kupitia Ziwani. Kuhusu mradi wa barabara zinazoendelea ambazo zinagharimiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Zanzibar, *Saudi Fund* na *BADEA* imehusisha barabara 3.

Barabara ya Wete - Gando, barabara ya Wete – Konde na barabara ya Wete – Chake chake. Mhe. Spika, hatua zinazoendelea ni kuwa utekelezaji wa mradi huu umegawika katika mafungu mawili. Mhe. Spika, awamu ya kwanza ya mradi inahusisha ujenzi wa barabara ya Wete hadi Konde na Wete hadi Gando. Kazi ya utekelezaji ya awamu hii ya mradi imeanza na inaendelea vizuri.

Mhe. Spika, awamu ya pili ya mradi huu utahusisha ujenzi wa barabara ya Wete hadi Chake chake kupitia Ziwani utekelezaji wa barabara hii utafanywa mara tu baada ya kufikia hatua nzuri za ujenzi wa barabara ya awamu ya kwanza, fedha za ujenzi huo zipo na serikali itahakikisha kuwa barabara hii itajengwa ili kuwarahisishia usafiri wananchi na watumiaji wa barabara hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, naomba kuelimishwa zaidi kuhusu *feeder road* kwa sababu njia zote anazozitaja sio njia za wananchi zinazokwenda kwenye majumba yao, lakini ni njia za kwenda vijijini na njia moja inakwenda katika makao makuu ya umeme unaotoka Tanga kule Mkumbuu. Kwa hivyo, naomba wizara inielimishe hiki kifungu cha tatu kwa nini njia hizo zikaingia katika kifungu cha 3 na sio kama ni *feeder road.*

b) Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anihakikishie kwa sababu njia inayotoka Mchangawakwale hadi Pembeni wananchi inaponyesha mvua hawatoki wala hawaingii kwa gari yoyote ile hata trekta haliendi. Je, ananihakikishia kwa sababu tuko Januari mwezi wa Machi utakapofika njia hiyo itakuwa imeshatiwa fusi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika suala mama na jibu mama kuna aina nyingi za barabara lakini yeye anataka kuelimishwa maana ya *feeder road*.

Mhe. Spika, *feeder road* ni njia yoyote ile iwe ya miguu, iwe ya baiskeli, iwe ya gari lakini inayoingia ama katika barabara kuu na hizo barabara kuu ziko

nyingi, kuna *motor way*, kuna *high way* kuna *main road*. Kwa hivyo, barabara zote ambazo zinachangia kuingia barabara kuu hizo ni *feeder road* lakini katika ujenzi wa barabara hizi zinagaiwa makundi. Kwa hivyo, kwanza maana ya *feeder road* ni njia yoyote inayoingia katika njia kubwa.

Mhe. Spika, hizi barabara ambazo zimetajwa humu ni 6 zina urefu wa kilomita 25 na kwa gharama za siku hizi kiasi kinachotakiwa kujenga barabara hizi ili ziwe *roads* pamoja na lami na kila kitu zitagharimu angalau bilioni 25. Kwa hivyo, tuliposema kwamba kuna barabara ambazo serikali kwa mujibu wa *Act* zinazishughulikia ni hizo barabara ambazo zimetajwa na ndizo hizo ambazo zimejengwa. Lakini haina maana kwamba barabara nyengine zote zile zilizomo vijijini serikali haina wajibu, serikali maana yake inajumlisha hata Serikali za Mitaa tuna Halmashauri za Wilaya. Mhe. Spika, Halmashauri za Wilaya kuna Mabaraza ya Mji Wete, Chake-Chake na Mkoani na hapa tuna Manispaa ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ilivyo hasa ni kwamba barabara zote zilizoko katika Manispaa ya Zanzibar wajenge Manispaa na barabara zilizoko vijijini katika Halmashauri zijengwe na Halmashauri. Mhe. Spika, serikali kama serikali Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wajibu wake ni kujenga barabara hizi ambazo tumezungumza zinatafutiwa wafadhili kama alivyosema kuna barabara ya Wete – Konde, Wete – Gando na Wete – Chake-Chake mfadhili ni *BADEA*, *Saudi Fund* na SMZ. Mhe. Spika, hizo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni kwamba barabara mbili zinajengwa kwa mpigo na pamoja na matatizo ambayo ni ya kawaida kwa ujenzi wowote sisi tunaweza tukasema kwamba inakwenda vizuri ukilinganisha na barabara nyengine.

Mhe. Spika, nikisema kwenda vizuri mambo ya ujenzi wa barabara ni kama mafya matatu, mafya mawili hayawezi kuteleka chungu, kuna mjenzi *contractor,* kuna serikali au *client* na kuna anayetoa fedha kwa ajili ya ujenzi. Kwa hivyo, hawa watatu lazima waende kwa pamoja kama mjenzi hajalipwa kwa mujibu wa mkataba basi serikali ikilaumu, mjenzi anaonesha kidole kwamba mimi siwezi kuendelea kwa sababu hujanilipa. Mhe. Spika, pamoja na yote mimi nasema ukichukua mambo haya matatu mjenzi, mjengewa na anayetoa fedha barabara zile mbili zinakwenda vizuri na nina hakika sherehe zinazokuja za Mapinduzi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itakuwa ni nambari moja kwa ufunguzi wa barabara nyingi zaidi ya barabara saba zitafunguliwa, zikiwemo hizo mbili.

Mhe. Spika, sasa nirudi kwenye suala la pili ni kwamba barabara anayosema kutoka Mchangawakwale mpaka Pembeni mimi mwenyewe juzi nimepita gari sasa hivi inapita. Mhe. Spika, ni kwamba siwezi kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba katika kipindi hicho anachosema barabara hii itakuwa

imewekwa kifusi. Ninachoweza kusema ni kwamba tunaomba fedha kutokana na *road fund*, *road fund* haiko chini ya wizara yetu iko chini ya Wizara ya Fedha kama Mhe. Mwakilishi atakwenda kuzungumza na Mhe. Waziri wa Fedha ili *road fund* itupe fedha kiasi nakuhakikishia tutaitia kifusi mle mwahali ambamo mmeharibika ili wakati huu wa masika watu wa Pembeni wasichukuliwe tena kwa vitanda na wengine wakafa njiani. Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi moja ya nyongeza. Mimi ninataka zaidi anisaidie kuhusu barabara yangu ya Kuukuu Kangani. Mhe. Spika, kwa kuwa barabara ya Kangani Kuukuu imo katika orodha ya kutengenezwa lakini barabara ile sasa hivi imekuwa ni tatizo kubwa sana haipitiki wakati wa mvua wala jua. Je, Mhe. Waziri ni msaada gani utakaowasaidia wananchi wa Kangani ili waondokane na tatizo lile.

Mhe. Spika: Tumsaidie swali lake Mhe. Waziri ingawa liko mbali kidogo.
Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, nimemfahamu vizuri Mhe. Mwanajuma Faki. Barabara anayoizungumzia Mheshimiwa ni kutoka Kangani mpaka Kuukuu. Yote hiyo ni Kangani lakini ni vijiji tu. Barabara hii ina urefu wa kilomita 1.7, ni juzi tu ambapo nimefanya ziara barabara hii sisi tumeweza kupita katika hali ngumu ni kweli, wakati wa mvua haipitiki wakati wa jua hifikiki.

Kutokana na hali ilivyo barabara hii haimo katika ujenzi wa *NORAD* na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini imo katika mradi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar peke yake ya barabara inayotoka Mkanyageni kwenda Kangani. Lakini kwa hali mbaya ilivyo kipande hicho cha kilomita 1.7 tumekubaliana na Idara ya UUB Pemba kwanza kufanya huduma ya mwanzo (*first aid).* Sasa hivi wanaishughulikia barabara inayotoka Mtambile kwenda Kangani, kabla hawajamaliza kazi basi kipande kile kidogo kinachotoka Kangani kwenda Kuukuu kiwe kimewekwa sawa na zile sehemu ambazo zinahitaji ukarabati wa kuwekwa kifusi tutaweka.

Kwa hivyo, namhakikishia Mhe. Mjumbe hii naisimamia mwenyewe na kama mvua za masika zitanyesha kabla ya tarehe 1 Machi, 2011 basi njia itakuwa haipitiki, lakini kama mvua zitanyesha baada ya tarehe 3 Machi, 2011 basi ataweza kupita kwa gari tena kwa mwendo anaotaka katika barabara hiyo.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, nadhani muda wa maswali umekwisha. Tuna tatizo kwamba maswali majibu yake ni marefu kidogo, ningeomba maswali ya msingi yenyewe yawe mafupi yanayoeleweka, lakini na majibu yawe mafupi yenye ufafanuzi mzuri. Itatusaidia kuokoa muda ili tutapoendelea na shughuli zetu hizi maswali yanayoulizwa na Waheshimiwa

Wajumbe tupate kuyamaliza. Leo nadhani tumebakiwa na bakaa ya maswali matano hivi ambayo hayakujibiwa na yalipangwa yote yaweze kujibiwa leo. Sasa tutakapoendelea kwa siku za usoni niwaombe Waheshimiwa Wajumbe na Waheshimiwa Mawaziri kujaribu kuuliza maswali kwa kifupi na majibu yakawa kwa ufupi lakini yenye kutoa ufafanuzi mzuri. Nashukuru tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

MAREKEBISHO YA KANUNI YA BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu katika Baraza letu la Wawakilishi la wananchi wa Zanzibar. Aidha, napenda nikushukuru wewe kwa busara na hekima zako za kunipanga kuwa mtu wa kwanza kwenye mkutano huu kufanya uwasilishaji wa hoja hii ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, nakushukuru sana Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe.

Vile vile naomba nitoe pongezi zangu za dhati na shukurani nyingi kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mhe.. Ali Abdalla Ali ambayo ilifanya kazi kubwa kuyapitia mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni zetu za Baraza neno kwa neno na kwa kutusaidia vya kutosha kwa kutupa ushauri, maoni ambayo kwa kiasi kikubwa yamechangia kuyafanya marekebisho haya yanayopendekezwa yawe mazuri zaidi.

Aidha, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu ambao walishiriki kwa pamoja kwenye warsha iliyofanyika siku ya Jumapili tarehe 16 Januari, 2011 kuhusu marekebisho haya ya Kanuni za Baraza. Kwa kweli warsha ile imenirahisishia kazi ndani ya Baraza hili kwani maoni yote ya Wajumbe yamefanyiwa kazi kama tulivyokubaliana na katika warsha ile yamejumuishwa kwenye marekebisho haya ambayo yanapendekezwa.

Mhe. Spika, napenda nitoe shukurani zangu maalum kwa Katibu wa Baraza na watendaji wake kwa namna ambavyo wamenipokea na ushirikiano mkubwa walionipa katika kuandaa rasimu ya marekebisho haya ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe Kanuni za Baraza la Wawakilishi zimetungwa chini ya kifungu 86(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa shabaha na madhumuni na malengo ya kurahisisha na kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi. Kanuni hizo zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya usimamizi na utekelezaji wa kazi za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe kanuni zetu zinazotumika hivi sasa ni toleo la mwaka 2009 na kutokana na mabadiliko yaliyotokea imelazimika kanuni hizo zifanyiwe marekebisho, kabrasha ambalo mnalo yamo marekebisho ya Waheshimiwa ambayo yanagusa maeneo manne makubwa.

1. Marekebisho yanayotokana na kuanzishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa.
2. Hali halisi ya uzoefu wa uendeshaji wa mabunge katika nchi za Jumuiya ya Madola.
3. Uzoefu uliopatikana katika uendeshaji na utekelezaji wa shughuli za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.
4. Madhumuni ya Kurekebisha lugha, makosa ya kiuchapaji na kuweka mtiririko mzuri wa maana na kurahisisha ufahamu na mpangilio mzuri wa nambari.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu likubali kufanya marekebisho kwenye Kanuni zetu za Baraza kama ilivyooneshwa kwenye kabrasha tulilowapatia. Mimi naomba kusema kwa muhtasari kwa yale maeneo ya msingi yanayopendekezwa kurekebishwa kwenye kanuni zetu.

Mhe. Spika, nianze kwa kanuni ya pili. Katika kanuni ya pili kuna marekebisho yanayohusu tafsiri na ufafanuzi kama ifuatavyo:-

> Maneno mapya yanayoingizwa na kufafanunuliwa na tafsiri yake ni Makamo wa Rais, Naibu Waziri, Mnadhimu Mkuu wa Serikali na Mnadhimu wa Vyama. Baadhi ya maneno yanafutwa yakiwemo ya Mkuu wa Mkoa, Mnadhimu wa Chama Tawala, Mnadhimu wa Upande wa Upinzani. Baadhi ya maneno yanayorekebishwa na tafsiri yake. Katika neno ‘Kamati’ kuondoa maneno ‘Kamati za Vipindi’. Katika maneno ya ‘Viongozi wa Baraza’ kuingiza maneno ya ‘Mnadhimu Mkuu wa Serikali’.

Mhe. Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika kanuni ya tano yanahusu uchaguzi wa Spika na ni kama ifuatavyo:-

1. Fomu za uteuzi wa wagombea Uspika zirejeshwe kwa Katibu wa Baraza angalau saa 24 kabla ya uchaguzi wa Spika badala ya saa 48 kama ilivyokuwa awali.

2. Idadi ya Wajumbe wa Baraza wa kumuunga mkono mgombea Uspika inabaki ile ile ya watu watano, lakini inatolewa nafasi kwa mgombea kuweza kuungwa mkono na watu watano wasio wajumbe wa Baraza, lakini wenye sifa za kugombea ujumbe wa Baraza.

3. Wagombea wa nafasi ya Uspika wapewe nafasi ya kujieleza kwenye Baraza na kuulizwa maswali yasiozidi matatu kwa kila mgombea.

4. Kazi ya kuhesabu kura ya Uspika ifanywe bila ya kushirikishwa mjumbe kutoka Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, marekebisho ya kanuni ya 12 yanahusu wajumbe kugawika pande mbili yanarekebishwa kama ifuatavyo:-

Wajumbe watagawika pande mbili ambazo ni upande wa Mawaziri, Manaibu Waziri na Mwanasheria Mkuu na wajumbe wasiokuwa Mawaziri, Manaibu Waziri na Mwanasheria Mkuu itakuwa ni upande wa pili. kabla ya hapo maeneo haya ilikuwa ni upande wa chama tawala na upande wa upinzani.

Mhe. Spika, kanuni nyengine inayofanyiwa marekebisho ni kanuni nambari 13 kwa kumtambua Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuwa ni kiongozi wa shughuliza serikali kwenye Baraza kama alivyotajwa katika Katiba kwenye kifungu cha 39(7) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Toleo la mwaka 2010, kabla ya hapo kifungu hiki kilimzungumzia Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, kanuni nyengine tunazorekebisha ni kanuni ya 14, 15 na 16 zinarekebishwa kwa madhumuni ya kuanzisha nafasi ya Mnadhimu Mkuu wa Serikali. Mnadhimu wa Chama Tawala na Mnadhimu wa Upinzani nafasi hizo sasa zinafutwa na kuwa sasa tutakuwa na wanadhimu wa vyama.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, kanuni nyengine ni kanuni ya 18 inayohusu Mshauri wa Baraza, inarekebishwa kwa kuainisha wazi wazi kwamba Mshauri wa Baraza awe ni Mwanasheria mwenye uzoefu usiopungua miaka saba, hapo awali ilisema ni mwanasheria mwenye uzoefu wa kutosha.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kanuni nyengine inayorekebishwa ni ya 27 inayohusu dua, inarekebishwa kwa kuitaja Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa

kifungu cha Katiba. Kabla ya hapo ilisomeka Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe waliofanya marekebisho haya.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, kanuni ya 33 inayohusu hati za kuwasilisha mezani inarekebishwa ili kupewa nafasi kwa Naibu Waziri aweze kuwasilisha hati mezani kwa niaba ya Waziri. Aidha, marekebisho ya kanuni hii yanafuta maneno Waziri Kivuli na sasa Mwenyekiti wa Kamati atatoa maoni yake.

Mhe. Spika, kanuni nyengine tunayoirekebisha ni ya 44 inayohusu kauli za Mawaziri, nayo inarekebishwa hivi sasa kutoa nafasi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya sekta husika kutoa maoni ya kamati kuhusu kauli hiyo. Kabla mapendekezo hayo ilikuwa ni Waziri Kivuli ndiye hutoa maoni kwa upande wa upinzani kuhusu kauli hiyo.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kanuni nyengine inayorekebishwa ni kanuni ya 59 inayohusu mambo yanayofaa na yasiofaa kuzungumzwa kwenye Baraza. Inarekebishwa ili kukataza kutumia jina la Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa dhihaka au kwa madhumuni ya kutaka Baraza kuamua jambo lolote kwa namna fulani au kuzungumzia mienendo yao. Hapo kabla ilikatazwa kutumia jina la Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe marekebisho mengine ni kanuni ya 91(2) inayohusu nakala ya Mswada unaopitishwa na Baraza, nakala ambayo inapelekwa kwa Mhe. Rais ili kupata kibali chake kitakuwa katika lugha ya Kiswahili na pia katika lugha ya Kiingereza.

Marekebisho haya yanafanywa ili kukidhi maelezo na matakwa ya kifungu cha 87 cha Katiba ya Zanzibar. Kwa sababu Mhe. Spika, mwanzoni tulikuwa tunapeleka nakala moja tu ya Kiswahili. Sasa kwa ajili ya kusaidia na shughuli za Kimahakama tunapeleka nakala mbili, moja ya Kiswahili kwa mujibu wa Katiba na moja isaidie matumizi ya Mahakama ambayo itakuwa ya Kiingereza.

Mhe. Spika, kanuni nyengine ni ya 93 (9) inarekebishwa ili kufuta ule utaratibu wa kumpa nafasi msemaji wa upinzani, kutoa maoni ya upande wa upinzani juu ya makadirio ya bajeti ya serikali na bajeti ya kila wizara.

Mhe. Spika, kanuni nyengine ni ya 95 inayohusu muda wa kufikiria makadirio ya wizara mbali mbali kwenye Baraza, inarekebishwa kwa kuongeza muda huo kutoka siku 30 na kuwa siku 35. Hii inatokana na ongezeko la wizara kutoka 13 na kuwa 16.

Mhe. Spika, kanuni ya 96 inarekebishwa kwa kufutwa fasili ya 5(c) ya kanuni hiyo. Marekebisho haya yanakusudiwa kuwa tubakie na uondoshaji wa shilingi moja endapo mjumbe hakubaliani na matumizi ya kifungu maalum, au kupunguza shilingi mia moja ikiwa mjumbe anaashiria kutoridhika na sera. Kwa hivyo, kupunguza kiasi maalum katika fungu inafutwa.

Mhe. Spika, kanuni ya 104 inarekebishwa kwa kuanzishwa Kamati za Kudumu za Baraza mbili mpya ambazo itakuwa ni Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na ya pili Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Hii inakidhi haja ya wizara ambazo zimeanzishwa. Vile vile jina la iliyokuwa Kamati ya Fedha na Uchumi linabadilishwa na sasa itakuwa ni Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Na kamati nyengine zitabaki na majina yake kama ilivyokuwa awali.

Mhe. Spika, kanuni ya 107 inayohusu muundo wa kamati ya uongozi na shughuli za Baraza inarekebishwa kwa kumuondoa kiongozi wa upinzani na badala yake kuwaingiza wanadhimu wa vyama. Marekebisho haya pia yanamuondoa Waziri Kiongozi na kumuingiza Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kanuni ya 135 inarekebishwa ili kuweka utaratibu mpya wa ukaaji wa wajumbe wa ndani ya Baraza ambapo mawaziri watakaa safu ya mbele bila ya kuzingatia vyama vyao na mfano mzuri Mhe. Spika, ni kama huu ambao tayari waheshimiwa wamekaa wakifuatiwa na Manaibu Waziri na wajumbe wengine watakaa safu zinazofuata bila ya kuzingatia vyama vyao.

Mhe. Spika, marekebisho mengine ni ya kanuni ya 141 kuhusu utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe watatu wa Baraza kwenda Bungeni, yameondoa yale maneno ya chama tawala na upinzani tu. Lakini utaratibu unabaki ule ule wa kugawana nafasi hizo kwa njia ya uwiano wa vyama vya siasa vilivyomo kwenye Baraza. Aidha, marekebisho mengine yanayopendekezwa katika kanuni hii ni kuondoa ulazima wa kuleta majina matatu kwa kila nafasi kutoka kila chama cha siasa chenye haki ya kuleta wagombea wa nafasi za ubunge.

Mhe. Spika, sasa chama cha siasa chenye haki ya kuleta wagombea kwa nafasi ya ubunge kitaruhusiwa kuleta jina moja ama majina kama itakavyoona inafaa lakini yasizidi matatu.

Mhe. Spika, kanuni ya 143 inayohusu Tume ya Bajeti ya Baraza inarekebishwa kwa kumuondoa kiongozi wa upande wa upinzani na badala yake kumuingiza Mnadhimu Mkuu wa Serikali. Pia wanadhimu wa vyama wanaingizwa wawe wajumbe wa Tume ya Bajeti, vile vile Katibu Mkuu Fedha anaingizwa kuwa Mjumbe. Aidha, inapendekezwa kuwa nafasi za Waheshimiwa Wajumbe watatu wa Baraza wanaochaguliwa na Baraza kuingia kwenye Tume ya Bajeti

ya Baraza mbali na kuangalia jinsia zigawiwe kwa kufuata uwiano wa vyama vya siasa vilivyomo kwenye Baraza. Lakini endapo chama au vyama vimegomea uchaguzi huo basi chama au vyama vitakavyoshiriki uchaguzi vitajaza nafasi hizo.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kanuni ya 151 inarekebishwa ili iendane na utaratibu unaotumika sasa katika kufanya marekebisho ya Kanuni za Baraza, yaani hoja ya marekebisho ya Kanuni za Baraza hupelekwa kwanza kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na baadae ndio huwasilishwa kwenye Baraza. Ilivyo sasa katika kanuni inaweza kutafsirika kwamba inatakiwa kwanza hoja hiyo iwasilishwe kwenye Baraza na baadae ipelekwe kwenye kamati. Hivyo, marekebisho haya yanasaidia kuweka ule utaratibu ulio mzuri zaidi.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yaliyomo kwenye kabrasha la mapendekezo ya marekebisho ni yale yanayohusu masahihisho ya lugha, makosa ya kiuchapaji na kuweka vizuri mpangilio wa nambari.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wayapokee marekebisho haya, wayatafakari na kuyajadili kwa kina na hatimaye wayakubali. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuhusu uwasilishaji mapendekezo na marekebisho ya kanuni za Baraza.

Mhe. Spika, awali ya yote nachukua fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake zisizo na kikomo kwetu ikiwa ni pamoja na kutujaalia uhai na afya njema, kiasi kwamba tumemudu kukutana hapa leo kujadili mambo mbali mbali yenye manufaa kwetu binafsi na kwa wananchi wetu kwa ujumla. Kwa hakika kama si taufiki na rehema zake Mwenyezi Mungu juu yetu, basi huenda muda huu tusingekuwa hapa tukipitia uwasilishaji wa mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Lakini kwa vile rehema za Mwenyezi Mungu zimeenea kwa waja wake, basi ndio maana muda huu tuko hapa tayari kujadili na hatimae kupitisha mapendekezo haya.

Mhe. Spika, pili napenda kuendeleza shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuniruhusu niwasilishe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Marekebisho ya Kanuni hiyo.

Mhe. Spika, wakati wa kupitia na kuchambua mapendekezo ya marekebisho katika kamati, nathubutu kusema kuwa kamati yetu ilipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed. Hivyo kamati inawashukuru wote hao kwa pamoja kwa mashirikiano mazuri waliyotupa kwa muda wote.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina wajumbe 8 ambao walihusika kikamlifu katika kupitia Kanuni hizi. Wajumbe wenyewe ni:

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Khamis Silima	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
8.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, Kanuni za Baraza la Wawakilishi zilitungwa chini ya kifungu cha 86(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa shabaha, madhumuni na malengo ya kurahisisha na kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza. Kanuni hizo zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya usimamizi na utekelezaji wa kazi za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, 2011 yamekuja kufuatia pamoja na mambo mengine, ni kurekebisha baadhi ya kanuni za kanuni hiyo ili kukidhi haja kwa muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Umoja wa Kitaifa iliyoundwa baada ya uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2010.

Mhe. Spika, kamati yetu haina pingamizi na mapendekezo yaliyotolewa na Afisi ya Baraza, hii ni kutokana na kuwa marekebisho haya yaliyofanywa yataliwezesha Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu yake kwa kufuata muundo huo mpya wa serikali. Mhe. Spika, baadhi ya kanuni zilizorekebishwa ni:-

Kanuni ya 2 kwenye tafsiri za maneno **"Mnadhimu wa Chama Tawala"** na **"Mnadhimu wa Upande wa Upinzani"**, na imependekezwa tafsiri hizo zisomeke kuwa ni **"Mnadhimu wa Chama"**. Aidha, kwa kuwa Makamo wa Pili wa Rais ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali na ni Msemaji Mkuu wa Serikali ndani ya Baraza kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, imependekezwa kufutwa maneno **"Waziri Kiongozi"**, kwa zile Kanuni zinazohusiana moja kwa moja na majukumu ya Kiongozi huyu.

Mhe. Spika, Kanuni hizo ni:-

Kanuni za 13(1) na 106(1)(i). Ama kwa zile Kanuni zilizomtaja **"Waziri Kiongozi"** na zikamjumuisha pia na Makamo wa Kwanza wa Rais, basi Kanuni hizo zimependekezwa zisomeke; **"Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais"**. Kanuni zenyewe ni kanuni za 57(6), 57(7), 123(1), 123(2), 126 na 127(1).

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaunga mkono marekebisho ya Kanuni ya 12 inayohusu wajumbe kugawika pande mbili. Hapo kabla wajumbe waligawika pande mbili kwa kuzingatia tofauti za vyama vyao, yaani Upande wa Chama Tawala na Upande wa Upinzani. Mhe. Spika, marekebisho ya kanuni hiyo yameondosha mgawanyiko huo na badala yake imependekezwa wajumbe kugawika pande mbili kwa kuzingatia nafasi zao walizokuwa nazo.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, Kanuni ya 135 inayohusiana na ukaaji wa wajumbe ndani ya Baraza, inadhihirisha kuwa Baraza la Wawakilishi linazidi kuyaheshimu mawazo ya wananchi wa Zanzibar juu ya kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hii inatokana na kuwa ukaajii huo mpya uliopendekezwa utawawezesha Wajumbe wa Baraza kukaa ndani ya Baraza bila ya kujali tofauti zao za vyama.

Mhe. Spika, napenda kuwatoa wasiwasi wananchi wa Zanzibar kwamba ukaaji huo mpya ndani ya Baraza haumaanishi kuwa Baraza la Wawakilishi halitakuwa tena na jukumu la kuisimamia serikali, la hasha. Jukumu hili bado lipo na litasimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Spika, tunapongeza pia marekebisho ya kanuni ya 18 ya Kanuni za Baraza inayopendekeza kwamba Mshauri wa Baraza lazima awe ni Mwanasheria mwenye uzoefu usiopungua usiopungua miaka saba.

Mhe. Spika, tunalipongeza hili kwa kuwa litaweka uwiano baina ya mihimili mikuu ya Dola. Hapa ninamaanisha kwamba ni busara kwa Mshauri wa Baraza kuwa na uzoefu wa mwanasheria kwa kipindi hicho kama ilivyo katika uzoefu

wa masuala ya sheria kwamba kipindi hicho cha uteuzi wa Majaji au Mwanasheria Mkuu huwa wanachukua miaka hiyo saba. Hii ni kutokana na kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 94(iii) ya Katiba ya Zanzibar, mtu atakayefaa kuwa Jaji au Kaimu Jaji wa Mahakama Kuu mpaka pamoja na sifa nyengine awe na uzoefu usiopungua miaka saba.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 55(2) cha Katiba ya Zanzibar, mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Mwanasheria Mkuu au kufanyakazi za Mwanasheria Mkuu mpaka pamoja na sifa nyengine awe na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka saba.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala haina pingamizi na Marekebisho ya Kanuni ya 91(2) inayohusiana na kupelekwa nakala ya Mswada wa Kiswahili kwa Mheshimiwa Rais ili kupata kibali chake. Mhe. Spika, hatua hii itaiwezesha Nchi yetu kuzidi kuonekana kuwa inatii matakwa ya Katiba tuliyoitunga wenyewe. Hii ni kutokana na kuwa, hapo kabla Mhe. Rais alikuwa anapelekewa Miswada ya Kiingereza jambo ambalo ni kinyume na Kifungu cha 87 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, pamoja na Kuimarisha Utawala Bora na Misingi ya Utoaji Haki.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, hatua hii muhimu itaondosha usumbufu kwa wananchi wa kawaida, kwani tunakiri kuwa maneno *"terminologies"* za kisheria ni za kitaalamu zaidi *"very technical".*

Hivyo, Kamati yetu inashauri ni busara Mheshimiwa Rais akatia saini nakala zote mbili za Miswada yaani Mswada wa Kiswahili na wa Kiingereza.

Mhe. Spika, eneo jengine muhimu ambalo limefanyiwa marekebisho ni kuanzishwa Kamati za Kudumu za Baraza mbili mpya ambazo ni;- (i) Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. (ii) Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari".

Mhe. Spika, hatuna pingamizi na hili kwani litaleta ufanisi ulio bora zaidi katika Kamati za Kudumu za Baraza zinapotekeleza majukumu yake. Aidha, linaweza kuondosha malalamiko kuwa muda unaopewa Kamati kutekeleza kazi zake kuwa ni mdogo.

Mhe. Spika, Marekebisho mengine yaliyomo kwenye waraka wa Mapendekezo ya Marekebisho ni yale yanayohusu masahihisho ya lugha, makosa ya kiuchapaji na kuweka vizuri mpangilio wa nambari ili Kanuni za Baraza la Wawakilishi ziweze ueleweka zaidi. Kamati yetu inayaunga mkono marekebisho yote hayo.

Mhe. Spika, namalizia hutoba yangu kwa kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini. Pia, nawashuru Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano yao mazuri waliyonipa. Aidha, nakushuru wewe Mheshimiwa Spika kwa mara ya pili kwa kuniruhusu kutumia muda mrefu kiasi kuwasilisha maoni ya Kamati yetu.

Mwisho kabisa napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naunga mkono Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar asilimia mia moja.

Mhe. Spika**,** naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa uwasilishaji huo sasa tuendelee na uchangiaji wa jumla.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi naomba nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwanza kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, zinazotoka moyoni kabisa kwa kutujaalia uhai na uzima kukutana hapa kwa kuanza shughuli rasmi za baraza hili.

Pili nikushukuru na wewe kwa kuniona na kunipa nafasi hii ya kwanza kuichangia hoja hii ambayo ipo mbele ya Baraza hili, mimi sitokuwa na mengi sana kwa sababu kama alivyosema tumeuchangia vya kutosha hoja hii katika kamati, lakini naomba nitumie fursa hii kuipongeza sana serikali na hasa Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kazi nzuri aliyoisimamia ya kuhakikisha kwamba marekebisho mengi yaliyofanywa yameingizwa hii ni dalili nzuri na dalili ya serikali sikivu. Inshaalla tunaomba utaratibu huu uendelee sio kwa hoja ya kanuni tu lakini kwa hoja nyingi ambazo zitakuwa zikichangiwa wa wajumbe kupitia katika kamati za baraza lakini pia kupitia katika ukumbi huu wa baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo kuna marekebisho ambayo yamefanyika nadhani yamefanywa katika warsha ambayo mimi sikupata nafasi ya kuhudhuria baada ya kujadiliwa na kamati, hayo ndio ambayo ningependa kuyachangia.

Moja ni katika kifungu cha 4 cha marekebisho haya ambacho kipo ukurasa wa pili pale, katika kufungu cha 4b kinapendekeza fasili ya 5c mstari wa nne unarekebishwa kwa kufutwa maeneno 48 na badala yake yasomeke 24 lakini naongeza pale.

Aidha mstari wa pili kutoka chini yanaongezwa maneno au watu watano ambao sio Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini wana sifa za kugombea ujumbe

wa baraza. Mimi hili kidogo linanipa wasi wasi tulilijadili kidogo katika kamati na kulikuwa na maoni tofauti lakini hatimae haya ambayo yameletwa hapa yananipa wasi wasi kwa sababu moja. Shughuli za Baraza la Wawakilishi ni shughuli za wajumbe wa baraza hili, katiba imeweka fursa au haki kwa mwananchi yoyote wa Zanzibar ambae ametimiza sifa zilizotajwa kugombea nafasi ya Spika.

Sasa kanuni imeweka utaratibu huo wa uchaguzi na huko nyuma ilikuwa ni kwamba mgombea anatakiwa adhaminiwe na wajumbe wa baraza, tulikuwa tukijadiliana sana kwenye kamati juu ya idadi hii ya wajumbe hasa kutokana na idadi ambayo ilikuwa ikitolewa na wagombea ambao vyama vyao haviwakilishi katika baraza hili.

Mhe. Spika, sasa hili lililokuja hapa linanipa shida kwa sababu moja tu hapa inasemwa sasa anaweza kudhaminiwa na wajumbe wasiopungua watano au watu watano ambao sio wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini wana sifa za kugombea ujumbe wa baraza. Tatizo langu lipo yupi au chombo kipi kitasimamia kuona kwamba hao waliodhamini wana sifa hizi naona baraza tunalitia katika msuko suko ambao hauna sababu yoyote, kwa sababu inaweza kuja kuhojiwa mtu akiona sharti hili halikutimizwa akenda mahakamani tutatakiwa baraza tuthibitishe kwamba mtu alitimiza sifa hizi. Sasa katika uchaguzi wale waliopita wao wemeshapenda katika chungio la tume ya uchaguzi ambayo katika sheria wana jukumu la kuona kwamba mgombea anayegombea jimbo la Baraza la Wawakilishi ametimiza sifa za kikatiba za kumuonyesha kwamba huyu ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Sasa wale ambao wamepitia katika chungio la tume na wamepitia katika taratibu zote zile akiingia humu anathibitishwa kwamba ana sifa hizo, lakini hawa ambao wanakwenda kumchamini mgombea kutoka nje ambao wanasemwa kwamba wana sifa hizi, sisi tutathibitisha vipi watu hao waliomdhamini mgombea wa Spika, wanazo sifa hizi. Kwa hivyo nilikuwa naomba hilo kidogo tuliangalie upya au kama kuna utaratibu zaidi uliofikiriwa naomba nisaidiwe ili na mimi niweze kuridhika.

Mhe. Spika, jengine ni dogo tu nadhani ni la kibinaadam tu tulighafirika katika kamati nadhani kwa mtizamo wangu nadhani hapa tumeghafilika, nalo liko katika kifungu cha 8 cha mapendekezo au marekebisho yaliyoletwa ukurasa wa 3 wa waraka huu tuliopatiwa.

Hiki kinaligawa baraza hili katika pande mbili na kinasomeka wajumbe wa baraza wanaweza kugawika katika pande mbili rasmi katika upande wa Mwanasheria Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa upande mmoja na

wasiokuwa Mwanasehria Mkuu, Mawaziri na Manaibu Waziri kwa upande wa pili hapa nilikuwa naomba tufanye marekebisho madogo.

Kwanza katika kuwataja hawa nadhani au ningependa niseme hivyo kiitifaki kwanza wangetangulia Mawaziri kabla ya Mwanasheria Mkuu, lakini la pili tumemsahau Makamo wa Pili wa Rais hapa ambae nae ni sehemu ya upande wa serikali, zamani wakitajwa Mawaziri kwa sababu alikuwepo Waziri Kiongozi nikimjumuisha na yeye Waziri Kiongozi. Lakini sasa kwa wadhifa wake wa Makamo wa Pili wa Rais huwezi kumfananisha yeye na waziri mwengine kwa hivyo nilikuwa nataka kwa upande ule wa serikali iorodheshwe katika hii tafsiri yake kwamba itamjumuisha Makamo wa pili wa Rais.

Halafu katika kifungu cha 54 ambacho kiko ukurasa wa 16 hili sipendekezi au sina maoni kwa maana ya kurekebisha chochote hasa, lakini natumia fursa hii kuweka tahadhari ili kuja kutizama huko mbele katika kuboresha au kuimarisha utendaji katika baraza letu na mfumo mzima wa utungaji wa sheria. Hiki kinazungumzia kurekebishwa kwa kanuni ya 91 na kanuni hii ni ile inayohusu mswada baada ya kusomwa na kupitishwa kupelekwa kwa Rais na kutoa kibali chake.

Kifungu kidogo cha pili cha kununi hii kinasema nakala hiyo inaweza kuwa katika lugha ya Kiswahili au kiingereza, sasa humu tumerekebisha kusema kwamba na ikihitajika kwa lugha ya kiingereza. Maelezo mazuri ametoa Mhe. Waziri na sina tatizo nalo, nilitaka kutumia fasihi kidogo ni kwamba hili suala linapaswa kuzingatiwa tena na tena, suala la miswada kupelekwa katika lugha mbili kwa rais. Hoja iliyotumika ni nzuri kwamba wananchi kuielewa lakini pia ni lugha inayotumika katika baraza la Kiswahili.

Hapa nikisoma katika katika kufungu cha 87 kinatambua kwamba lugha rasmi ya Baraza la Wawakilishi ni Kiswahili, sasa hoja yangu mimi ni ndogo tu kwamba hili tulitizame kwa makini sana hasa katika *cession* Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo inadhamana ya kutafsiri hii miswada kutoka Kiingereza kuja katika Kiswahili, imezoeleka kwamba miswada mingi huandaliwa kwanza katika kiingereza halafu ikatafsiriwa kwa Kiswahili, mara nyingi kumekuwa na tatizo hapa la tafsiri yake kutokwenda sawa sawa.

Lakini la pili kuna *interpretation Act* ambayo inatambua kwamba sheria ya ni ile ya kiingereza tofauti na katiba ambayo inatambulika ile ya Kiswahili, lakini lugha inayotumika barazani ni ya Kiswahili. Kwa hivyo dhamira ya watunga sheria inaonekana katika lugha ya Kiswahili, sasa kuna tatizo ikija ikitokezea kwamba itafeli kwa zile zilizopelekwa haziwiyani sawa sawa, wakati huku *interpretation Act* inasema sheria ya *ascetic* ni ya kiingereza. Lakinu lugha ya

baraza hapa ni ya Kiswahili ambayo ina dhamira ya watunga sheria walipokuwa wakitunga suala lile ilikuwa ni lini.

Sasa kama unavyojua masuala haya yakifika pahala mtu akiona hakutendewa haki akenda Mahakamani kudai haki katika sheria tulizopitisha hapa mwisho wa siku itaangaliwa dhamira ya watunga sheria ambayo ilikuwa katika lugha ya Kiswahili, kwa hivyo nilikuwa nasema twende vizuri kwa sababu tunahitaji kuwa nazo zote mbili, lakini hiyo inahitaji kuimarisha utendaji wetu katika kuweka hizi tafsiri mbili au lugha mbili, au rasimu mbili zilizoletwa za miswada ile ya Kiingereza na Kiswahili ziwe zinakwenda sambamba na hazitofautiani hata kidogo ili kuitafsiri vyema dhamira hiyo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naomba kusema naiunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, na mimi naomba nichukue fursa hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha sote kuhudhuria katika kikao hichi, pili nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii angalau niweze kutoa mchango mdogo katika kuiboresha kanuni yetu ya Baraza.

Mhe. Spika, kwanza naomba nianze na kumpongeza Waziri kutokana na kazi kubwa sana aliyoifanya pamoja na *secretariat* na niipongeze *secretariat* ya Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa na ya umahiri kwa kutengeneza kanuni hii.

Mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwa vile tulikaa juzi tukaipitia kwa undani kanuni hii naomba tu nijikite katika kufungu cha 5 kinachohusu juu ya uchaguzi wa Mhe. Spika, mimi nafikiri ufike pahala tuweze kufikiria tena namna ya Spika, wetu anavyoweza kupatikana, tufikiri kwa sababu spika katika nchi hii ni kiongozi mkubwa ni kiongozi wa mihimili muhimu ya dola, lakini vile vile Spika, kama ilivyoelezwa anaweza kufanywa kama ni kaimu wa Rais kwa hivyo mtu akifikia hatua hii ujue ni mtu mzito. Sasa kwa saababu ni mtu mzito ni lazima tufikirie kwamba kufuatwa utaratibu wake wa kumpata tusiuweke kuwa ni utaratibu lege lege.

Mhe. Spika, ilizungumzwa kwamba lengo la kuviruhusu vyama vyengine kugombea nafasi hii ni katika kuimarisha demokrasia ya kweli, lakini vile vile ilizungumzwa kwamba hata wale wadhamini basi katika kutokuibana demokrasia turuhusu kwamba mgombea yoyote yule hawezi kuwa na wadhamini wananchi watano tu ambao wana sifa za kuingia katika Baraza la Wawakilishi, hii ni kuimarisha demokrasia na mimi naiunga mkono ingawa

demokrasia ilishatangazwa kwamba kila mtu ana uwezo wa kujiunga na chama cha siasa hiyo ni demokrasia kubwa sana.

Lakini vile vile vyama vilipewa fursa ya kusimamisha wagombea wawakilishi, vyama vilipewa fursa ya kusimamisha wagombea urais hiyo ni fursa kubwa sana iliyopewa vyama, sasa ilikuwa ni jukumu la kila chama kuhakikisha kwamba kinafanya kazi kubwa ya kuingiza wajumbe katika Baraza hili.

Kwa hivyo demokrasia haijabanwa ya kuviruhusu au kuruhusu watu waingie katika baraza hili na wagombea wao wawe ni wagombea wanaodhaminiwa na wajumbe wa baraza hili, lakini yote mimi nakubaliana kimsingi kwamba basi kila anayetaka kugombea agombee na adhaminiwa na watu watano ambao wana sifa ya kuwa ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Lakini Mhe. Spika, hiyo tukiiwacha hapo mimi nadhani itakuwa sasa tunakaribisha demokrasia vurugu kwamba mtu yoyote anayetaka uspika ende tu kwa wananchi watano wenye sifa, mimi nataka nikuhakikishie kwamba kwa jimbo la Chake Chake nitaleta wagombea kumi kwa sababu ni rahisi sana kumpata mtu ambae anataka kugombea uspika na akapata watu watano ambao ni wapiga kura na wenye wezo wa kugombea ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, tukubali kwamba watu wengi hawaingii katika nafasi hizi katika nia hasa ya kugombea uspika, tukichukua kipengele hicho basi tutapata watu ambao watakuja kuuza majina. Mhe. Spika, kuna taratibu nyingi sana za kuuza majina sasa mimi pamoja na yote ili kuepuka vurugu, kuepuka watu katika nafasi hii katika kuuza majina na kwa kuwa ni utaratibu uliowekwa na sheria nyingi za uchaguzi kwamba wagombea watoe kiasi fulani cha fedha, wagombea wenye nia ya kugombea udiwani nadhani walitozeshwa shs. 25,000/= na tume ya uchaguzi, wagombea urais walitoleshwa milioni moja, uwakilishi laki mbili.

Mhe. Spika, ile inafanywa makusudi kuondosha msongamano hata katika majimbo yetu kama tutafanya utafiti pamoja na kazi nzuri waliyofanya wawakilishi lakini wagombea uwakilishi walikuwa ni kidogo katika majimbo ukilinganisha na Bunge kwa sababu bunge walikuwa ni elfu hamsini, ilikuwa ni rahisi zaidi kugombea ubunge kuliko uwakilishi. Kwa hivyo kutoa laki mbili ukenda kuziweka pahala ambapo huna imani kwamba utapata inakuwa ni kazi kidogo.

Kwa hivyo hii hoja ya wagombea kuwataka watoe kiasi fulani cha fedha Mhe. Spika, nadhani ina mantiki sana na mantiki yake ni kupunguza lile wimbi na vurugu kwa mtu ambae hayuko makini katika kugombea, kwa hivyo pamoja na

masharti haya tuliyoyaweka lakini kwa kuzingatia ukubwa wa nafasi ya Spika kwa kuzingatia siku moja kuepuka watu wanaokuja kuuza majina, basi naomba tuweke kipengele hichi cha mgombea yoyote wa spika ambae pamoja na sifa nyengine. Lakini aweke kiasi fulani cha fedha kama ni *deposit* na itangazwe kuwa iwapo atakosa uspika na kama hakupata kura japo mbili maana yake milioni yake moja imeshakwenda na maji nadhani hiyo itatupunguzia vurugu.

La mwisho ambalo ni dogo Mhe. Spika, kanuni zetu za saa hazitoi fursa za watu kunywa chochote ndani ya ukumbi huu, nadhani mabunge mengine tunaona wajumbe wakinywa angalau maji kitu ambacho kwa kanuni zetu haituruhusu, ilikuja ikazungumzwa hiyo ikaonekana basi hata chupa ya maji inaweza kutumika kuwa ni silaha. Kitu ambacho kwa utamaduni huu tuliokuwa nao na utamaduni wetu wa Zanzibar sidhani kama tutakuwa tunatumia chupa kuzifanya kuwa ni silaha zetu waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Spika, tuzingatie hili suala la wajumbe kutoka hasa kwa mazingira yetu kwenda kutafuta maji pengine Kiembesamaki kwa sababu mazingira yetu tuliyokuwa nayo kuna siku ukumbi wako utakuja kukosa wajumbe, kwa hivyo naomba kwa mazingira ya sasa na hali tuliyokuwa nayo basi kanuni yetu ituruhusu wajumbe wetu angalau kupata maji. Wenzetu wabunge wamewekewa mpaka pipi kule kwa wale wajumbe wanaosinzia sinzia angalau kumung'unya mung'unya, naomba na hilo lizingatiwe katika kanuni ili isiwe ni tatizo ambalo linaweza kumfanya Mhe. Mjumbe akakosa kikao muhimu kwa ajili ya kwenda kutafuta maji.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii na naomba nitoe mchango wangu kwa hoja hii ya Mhe. Waziri, sio mchango mrefu lakini naomba nitoe baraka zangu kidogo.

Mhe. Spika, na mimi nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoonyesha umadhubuti, sio hili tu la kanuni lakini ameanza hasa katika kusimamia malalamiko ya wananchi katika maeneo ya viwanja Unguja na Pemba, akisikia atu kwamba kuna tatizo la kiwanja yeye asubuhi anafika kuangalia tatizo nini, kwa hili naomba nimpongeze Mhe. Waziri na naomba aendelee hivyo hivyo hayo ndio matakwa yetu kama wawakilishi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hoja hii ya kanuni mimi naomba niseme machache kama ifuatavyo. Kwanza katika Tume ya Bajeti ya Baraza inaonyesha kwamba itawakilishwa pamoja na Wajumbe watatu wa Baraza mmoja ni mwananchi. Mimi nahisi tume hii ya baraza inahusika na kupanga maslahi ya Baraza la Wawakilishi na ukiangalia mgawanyo ule kuna wataalam wengi kutoka Wizara

ya Fedha na baadae wao ndio baadae huwasilisha haya matakwa ya Baraza, sasa kwa mtazamo wangu naona wajumbe watatu wa baraza ni kidogo. Kwa sababu baraza ndio ambalo linataka kujenga hoja jinsi ya bajeti ya baraza hili, sasa ushauri wangu naona wajumbe ni kidogo na tungeondeza wakawa watano kwa sababu mimi simuhisabu Spika na Naibu Spika, kwamba ni moja katika sehemu ya baraza mimi nahisabu ni moja katika sehemu ya serikali.

Kwa hivyo hawa wajumbe watano kama wangetoka baraza basi wangewasiliahsa vizuri baraza kwa ajili ya kutoa hoja juu ya tume ya bajeti ya baraza, kwa hivyo katika ushauri wangu ningeomba kabisa kwamba mshauri wa baraza kwa sababu ni mwanasheria angekuwa ni mjumbe wa tume ya baraza, kwa sababu atashauri baraza kisheria katika masuala haya. Kwa hivyo mshauri wa baraza tungemuweka moja kwa moja kwamba ni mjumbe wa tume ya bajeti ya baraza ili kusaidia nguvu za baraza la wawakilishi kama tume yao.

Pili ni suala zima la majukumu ya kamati pamoja na maelezo mazuri ambayo Mhe. Waziri juzi aliyatoa lakini bado mimi hoja yangu ya kamati ya Fedha, kwa sababu kamati ya fedha kazi yeke ni kusimamia mipango ya kiuchumi ya nchi, sasa kuitengea kamati ya fedha kukagua tu Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo na Biashara na tukaja sekta kama uvuvi au utalii nadhani bado tuna jukumu kubwa sana ya uchumi wa nchi kwenye kamati hii.

Mhe. Spika, ushauri wangu kwamba kamati ya fedha kama sheria haisemi vyenginevyo au katiba haisemi vyenginevyo basi itembee wizara zote kama ilivyo *PAC*, ili maeneo ambayo yanahusu uchumi wan chi kama utalii na uvuvi kamati hii ikapata kuelekezwa kimipango na kisera, badala ya kuacha tu kamati ya Fedha ikaangalia maeneo machacho kama ya kilimo na yale ya fedha yenyewe.

Kwa hivyo mimi ushauri wangu ni kwamba kamati ya fedha ingeruhusiwa kutembea kama vile ilivyo *PAC* ili kuendelea kutoa ushauri wa mipango na sera za nchi.

Jengine ambalo ningelisema katika kifungu cha 79 nadhani hiki hakikufanyiwa mabadiliko lakini ukurasa wa 52, suala la kuambiwa mswada utatangazwa kwa siku ishirini na moja nap engine utawafika hao wajumbe kwa siku ishirini na moja. Lengo la kifungu hiki ni kamba wajumbe wanatakiwa wapate fursa ya kupata maoni ya wananchi na wataalam wengine, lakini ukiangalia mswada huu utaona kwamba umekidhi matakwa ya kanuni kwamba umechapishwa kabla ya siku ishirini na moja, lakini mimi ninavyohisi ni nadharia tu unaweza kuambiwa umechapishwa leo lakini tarehe inakuwa ya nyuma ili usikiuke kifungu hiki cha kanuni, lakini mjumbe unamfika muda mfupi sana, kwa mfano

mswada huu wa juzi umenifika hapa tarehe kumi na nne, siku nne kabla ya kikao cha leo cha baraza.

Sasa Mhe. Spika, wasi wasi wangu ni kwamba wachapishaji wa mswada wanaweka siku ishirini na moja ndani ya huo mswada kiasi cha kukizi tu hayo matakwa ya kanuni, lakini hauchapishwi kama ulivyo kwa mujibu wa sheria, kanuni zinasema kwamba mjumbe kama mswada haukumfika kwa siku ishirini na moja kama ilivyo kanuni nini hatua ya mjumbe katika mswada ule aukatae au aseme nini. Kwa sababu kanuni inasema mswada ufike hizi siku 21, mjumbe ameupata leo na jana nini hatua ya mjumbe hasa afanye nini. Kanuni nadhani ingesema mjumbe afanye nini katika suala hili la kanuni.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niseme kwamba utaratibu wa kumchagua Spika kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe lazima uzingatiwe, si vyema kwamba watu watano tu kuhusishwa kupiga kura wampendekeze mtu kuwa mgombea spika. Nadhani ni kweli kuna siku Baraza hili litakuwa watu mia wanagombea Uspika kwa sababu nafasi ile ni rahisi sana na Spika ni mtu mkubwa ambaye nadhani masharti ya kumpata Spika basi yangekuwa mazuri zaidi.

Leo masharti ya kumpata Mwakilishi yanakuwa madhubuti zaidi kuliko kumpata Spika. Nadhani hapa Mhe. Waziri angezingatia na baadae tukapata ufafanuzi mzuri katika hili. Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Spika, kwanza kabisa nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia katika kifungu cha 64 kanuni ya 104 kama ambavyo kinajieleza.

Mhe. Spika, pamoja na maelekezo mazuri ambayo mwenzangu aliyenitangulia alikwisha kunifilisi kidogo kwa ajili ya yale niliyotaka kuyazungumza, lakini pia nitarejea katika lile jina halisi la kamati yenyewe.

Katika mapendekezo ya juzi tulikwenda tukafika pahala tukasema kama ilikuwa tatizo ni jina basi jina mnaweza kulirejesha likawa Kamati ya Uchumi na Fedha kama ilivyokuwa mwanzo, tukitilia maanani ilivyokuwa uchumi wetu sasa unaingia katika wizara tofauti.

Kwa hiyo, tungeliomba basi hili jina bado lisomeke kwamba ni Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo itakuwa inashughulikia wizara hizi hizi tatu kama ilivyokuwa mwanzo. Kwa sababu kipengele ni uchumi na wale wachumi wenyewe wote wapo katika Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, naomba bado kamati iendelee kusomeka kwamba ni Kamati ya Uchumi na Fedha tukiwa bado tunasubiri kuangalia utaratibu wa kuyashughulikia yale mengine. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu mdogo kabisa. Mhe. Spika, pili nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuweza kuangalia kanuni zetu ili ziweze kwenda na hali halisi ya muundo wa serikali na hata utendaji wetu wa shughuli za Baraza kwa sasa hivi.

Mhe. Spika, mimi kuna eneo dogo tu ndio ambalo nataka nilizungumze ingawa na wachangiaji wa mwanzo walilichangia kwa kweli michango yao vile vile namuomba sana Mhe. Waziri izingatiwe.

Mhe. Spika, kabla sijenda hapo labda nitie nyama tu katika suala la wadhamini wa Spika. Mhe. Spika, nakubaliana na wenzangu kwamba bado tuendelee na utaratibu wetu ambao wadhamini ni vizuri wakawa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kama alivyosema Mhe. Jussa Ismail Ladu pale kwamba inawezekana kuna mgombea wa Uspika akaja akadhaminiwa na watu ambao kutoka nje kabisa.

Sasa inawezekana kukaja kukaanza kuwekwa pingamizi mwenzetu yule akaja akakosa wadhamini pengine pingamizi zikenda Mahakamani. Lakini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tayari wameshakuwa na sifa zote ambazo za kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa hiyo inakuwa haina matatizo.

Mhe. Spika, nafasi hii ni nyeti ikija ikiwa kwamba kuna kesi Mahakamani hamuwezi kumchagua Spika kwa hiyo hata utendaji wa shughuli za Baraza zinaweza zikakwama kidogo. Kwa hiyo, bado nilikuwa na mapendekezo kwamba wadhamini ni vizuri wakawa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, pia nataka kumshauri Mhe. Waziri katika marekebisho ya kanuni ya 142 ukurasa wa 29 katika hii karatasi tuliyopewa. Kanuni ya 94 ya 142 marekebisho yake. Hapa inasema kwamba fasili ya kwanza liongezwe neno “wasiozidi” baina ya neno “wajumbe watatu”. Hizi zaidi nakusudia katika nafasi zile za vyama vya siasa kuteua wagombea katika nafasi za ubunge.

Mhe. Spika, mimi nadhani hapa demokrasia tunataka kuibana, nafasi hizi kwa uelewa wangu pamoja na kwamba wajumbe wanatoka katika vyama lakini zaidi ni mali ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, tukija tukisema kwamba liongezwe neno “wasiozidi watatu” ina maana anaweza akaletwa mtu mmoja. Sasa hii nahisi kidogo inaweza ikaja ikanyima demokrasia.

Mhe. Spika, nitoe mfano mdogo, inawezekana labda mimi nimegombea ubunge pengine Mhe. Abubakar Khamis Bakary akawaambia wajumbe wake Mhe.

Hamza Hassan Juma msimchague. Sasa pengine katika chama changu nimeletwa mimi tu, hapa kidogo itakuwa imebanwa ile demokrasia. Lakini wakiwa watatu maana yake lazima tulazimishe kila nafasi igombewe na watu watatu. Kwa hiyo, ina maana pale wajumbe watakuwa na haki ya kuweza kumchagua yule ambaye wanahisi ataweza kuwawakilisha vizuri pengine ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Spika, nadhani hili tulikuwa nalo mwanzo tukafanya marekebisho sasa tunayarejesha tena. Kwa hiyo, mimi bado nashauri kwa kuwa nafasi hizi ni nyeti sana za kuwakilisha chombo hichi cha wananchi wa Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi ni vizuri bado demokrasia ikaachiwa ifanye kazi yake ili wajumbe sasa waweze kuangalia ni nani ambaye ataweza kuwawakilisha kuliko kuambiwa mchagueni huyu. Sasa hili kidogo itakuwa si utaratibu mzuri.

Vyenginevyo Mhe. Spika, nakubaliana na hoja za Mhe. Waziri pamoja na hayo marekebisho atakayoyafanya au atakayoyakubali pengine kupitia maoni mbali mbali waliyotanguliza Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba tena nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kujibu baadhi ya hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu marekebisho yetu ya kanuni.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa michango yao na ushauri wao ambao naamini tunazidi kuboresha kanuni zetu ili ziwe nzuri zaidi ziweze kusaidia utekelezaji wetu wa ndani ya Baraza uwe makini zaidi. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri ambayo waheshimiwa wametusaidia.

Mhe. Spika, nikianzia kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Ali Abdalla Ali kwanza ametupa pongezi. Napenda nitumie fursa hii kushukuru kwa kutoa pongezi hizo na kumhakikishia kwamba tunazipokea na tutaendelea kufanya kazi na kamati hii bega kwa bega ili tutekeleze majukumu yetu vizuri.

Mhe. Spika, mengi aliyosema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa niaba ya kamati yalikuwa ni kuzidi kuunga mkono yale mambo ambayo tumeyasema. Kwa hiyo, nisingependa kuyarudia isipokuwa nimshukuru kwa hekima na busara zao katika kamati na kumhakikishia kwamba haya tutayachukua tuyafanyie kazi kama ambavyo alivyotushauri.

Mhe. Spika, pili Mhe. Jussa Ismail Ladu pia napenda nimshukuru sana nae kwa ushauri na pongezi zake tunazipokea. Alizungumzia sana kanuni ya 5 kuhusu kudhaminiwa kwa Mhe. Spika na wajumbe wasiokuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Akataka kwa utaratibu huo basi, ili tuhakikishe kwamba wale wanaomdhamini Mhe. Spika, je, wanazo kweli sifa za kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, tunaomba kwa hili tufikirie, lakini nafikiri njia nzuri zaidi watu hao ni vyema wakachujwa na Tume yetu ya Uchaguzi kwenye kanuni zetu tukaonesha kwamba majina yale yatapelekwa kwenye tume kuhakikisha kwamba watu hawa wanazo sifa za kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili kupanua demokrasia zaidi tuwawezeshe na wenzetu wa vyama vyengine waweze kushiriki kikamilifu.

Kwa sababu nyote ni mashahidi wakati tukizungumzia hapa siku ya warsha, ilionekana kwamba mtu ambaye chama chake hakimo humu kwenye Baraza si rahisi kupata kudhaminiwa na Wajumbe wa Baraza letu tukufu. Kwa hiyo, ili kupanua hiyo demokrasia basi ikaonekana kwamba jambo hili nalo tulitafakari kwa kina na ndio maana ushauri wa wajumbe wengi ukaja kwamba tuwape nafasi basi wagombea hawa wapate nafasi za kudhaminiwa na watu wasiokuwa Wajumbe wa Baraza hili lakini wanazo sifa hizo.

Mhe. Spika, naamini kwa sababu watakaofanya kazi hiyo ni vyama vya siasa vitafanya kwa utaratibu mzuri na kwa kupitia tume tutasaidiana kuhakikisha kwamba basi watu hawa wanaruhusika.

Lakini ushauri alioutoa Mhe. Jussa Ismail Ladu kuhusu kumuingiza Makamo wa Pili wa Rais katika yale majina hilo ni jambo la muhimu kuwemo pale. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na ule mpango wa kuwa Makamo wa Pili wa Rais, Mawaziri, Mwanasheria Mkuu na Manaibu Mawaziri. Nakubaliana na hoja ile Mhe. Spika, katika kanuni ya 12.

Kuhusu kanuni ya 91 nafikiri ni vizuri vile alivyoshauri Mhe. Jussa Ismail Ladu kwamba uhitaji upo wa kuwa na nakala za lugha zote mbili ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa hiyo, ni vyema tukasema tu basi tunapeleka kwa lugha zote mbili kama ambavyo tumeshauri kwenye hotuba yangu ya awali ili kuondoa mgongano katika eneo hilo. Naamini itatusaidia, kwa hiyo tutahakikisha kwamba suala la tafsiri sasa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza iwe na maana sahihi na ile ambayo wajumbe waliionesha katika Baraza wakati wa kuchangia.

Tutahakikisha kazi hiyo tunaifanya ili tafsiri ioane kabisa na maana halisi, isijekuwa na maana nyengine katika kutafsiri kwenye lugha ya Kiingereza.

Maana lugha hii wakati mwengine inaweza kutoa tafsiri nyengine na ikaleta mvutano.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Omar Ali Shehe pia nae alizungumzia kuhusu hawa watu wenye sifa za kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Ni kweli kwamba fursa hizi wanaweza kujitokeza watu wengi kugombea hiyo nafasi ya Uspika. Lakini hapa kinapewa nafasi chama, chama cha siasa ndio kinaleta mgombea wake, sio kwamba kila anayejisikia atakuwa Spika anaweza kuja hapa kugombea Uspika.

Kwa hiyo, tunawapa fursa hii kwa vyama na naamini vyama vyetu viko *committed*, viko *serious*, vitafanya maamuzi yaliyokuwa *committed* katika kufanya jambo hili. Lakini moja ni hilo ambalo tunasema kwamba wale watakaodhamini tutawapeleka kwa Tume ya Uchaguzi ili waonekane kwamba wanazo hizo sifa.

Mhe. Spika, suala lile la ada itabidi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wazidi kutusaidia kwa sababu ni kweli umuhimu wa kulipa ada kwa atakayekuwa mgombea Uspika kuonesha *seriousness*, jambo hili lina umuhimu wake. Sasa hapa Mhe. Spika, tumia busara zako na uzoefu wako basi wajumbe watusaidie maana mimi nahisi kwa upande wangu suala la ada tunaweza kuweka kiasi. Kwa hiyo tuiachie afisi yako itafakari kiwango gani cha ada kitawekwa ili tuweze kuwa na ada na watakaojitokeza waonekane ni watu *committed* wana nia hasa ya kugombea nafasi hiyo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Omar Ali Shehe alizungumzia kuhusu suala la kupatikana kwa maji. Mimi nafikiri kanuni ya 61 (h) inatoa nafasi hiyo na kwa msingi huo basi Mhe. Spika, atatumia busara zake ili wajumbe wapate maji wasije kupata matatizo. Naamini afisi yako Mhe. Spika, itahakikisha mambo haya yanakwenda vizuri na chini ya uongozi wa wizara yetu pia tutashirikiana vizuri na Afisi ya Spika mambo yaende vizuri kuhakikisha kwamba busara zinatumika. Mhe. Spika, nina hakika kwa busara zako nyingi mambo haya yatakwenda vizuri tu.

Mhe. Spika, mchangiaji watu wa nne alikuwa Mhe. Hija Hassan Hija kwanza napokea pongezi zake, yeye alikuwa anazungumzia idadi ya Wajumbe wa Tume ya Bajeti. Alikuwa na wasi wasi kwamba wajumbe watatu ni kidogo, lakini mimi naona Mhe. Spika, wajumbe watatu wanatosheleza. Namuomba Mhe. Hija akubaliane na hayo kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wengi walikubaliana na hoja hii ya kuwa na wajumbe watatu. Naamini wajumbe watatu watatuwakilisha vizuri sana katika tume yetu ile. Lakini kama Baraza litaamua vyengine tutasikiliza ushauri wao.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Kamati ya Fedha kuwa na majukumu yaliyo sawa na *PAC* kidogo hapa linaweza kuleta migongano. Kamati ambayo ina uwezo kwa mujibu wa kanuni zetu iweze kutembelea wizara zote ingeendelea kuwa kamati yetu ya *PAC* na hiyo tuzidi kuiunga mkono tufanye hivyo.

Kuhusu jina hili kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wengi tokea mapema walikuwa wanapenda sana jina hili badala ya kuitwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo iendelee kuwa jina lile la zamani la Kamati ya Fedha na Uchumi.

Lakini kama tulivyosema awali na hoja kubwa ilikuwa ni kwamba ziko wizara nyengine ambazo nazo zinasimamia mambo ya uchumi. Kwa hiyo, ukiipa kamati moja jina lile la uchumi maana yake kama unafanya ile wizara nyengine nayo kuwa na ile rasilimali ya kuwa na wao ni wachumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kukubaliana kwamba kwa sababu hizi kamati hasa zinakuja kwa mujibu wa sekta zenyewe sasa tuzipe jina la sekta husika. Mhe. Spika, hapa itatusaidia zaidi kusimamia zile taratibu.

Mhe. Spika, mimi nazidi kushawishika kwamba kamati yetu ile jina lake ni zuri la Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kubakia hivyo na zile wizara nyengine zipate haki za kuwa nazo pia ni kamati za uchumi.

Kuhusu masuala ya miswada kucheleweshwa kwa mujibu wa siku 21 nataka nimhakikishie Mhe. Hija Hassan Hija wizara yangu kwa kushirikiana na Afisi ya Baraza la Wawakilishi sasa tutafanya kila njia kuhakikisha kwamba miswada inakuja kwa wakati na hatukiuki utaratibu huo wa kanuni, hatuna haja ya kuwekeana hatua zingine. Mhe. Hija naomba utupe nafasi tulifanyie kazi suala hili.

Mhe. Spika, tatizo letu kubwa ni kule *Printing Press* mashine zetu zimekuwa chakavu kuna matatizo sasa tunazishughulikia na serikali imechukua hatua ya kushughulikia jambo hili. Nakuhakikishieni kwamba mitambo ile Mhe. Spika, itashughulikiwa iwe mizuri ili itusaidie katika utendaji wetu wa kazi.

Mhe. Spika, mchangiaji wetu wa tano alikuwa ni Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, yeye pia yuko pale pale kwa sababu Mhe. Mahmoud ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Mhe. Mahmoud naomba tukubaliane kwenye hili kwa sababu hatupunguzi uwezo wa kamati kwa kutaja jina, uwezo na mamlaka yake unabakia pale pale. Tatizo ni kwa sababu ya sekta tu tusizidogoshe zile sekta zenyewe. Kwa hiyo, naomba tukubaliane tuendelee nalo jambo hili.

Mhe. Hamza Hassan Juma yeye bado alikuwa anaona kwamba kuleta jina moja kunakandamiza demokrasia kwa wale ambao watagombea nafasi ya ubunge kupitia Baraza letu tukufu. Nia yetu ni kwamba demokrasia hii tumeiachia vyama viamue kwa sababu kwa kiasi kikubwa nafasi hizi ni nafasi tumeziachia vyama japo ni nafasi za Baraza la Wawakilishi.

Kwa msingi huo basi, chama kama kitaona kitaleta zaidi ya jina moja, chama kina watu wengi zaidi, kina mjumuiko mkubwa zaidi, kina mawazo makubwa zaidi kuliko mtu binafsi. Kwa hiyo, tukiachia nafikiri busara za chama hii itatusaidia. Sasa nadhani yale mawazo ya jina kuanzia moja na yasiyozidi matatu ingetusaidia zaidi katika kutafuta ufumbuzi zaidi wa jambo hili na kupewa nafasi kubwa zaidi kwa chama.

Mimi naomba tukubaliane Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza letu tukufu hili kwamba kazi kubwa ya kanuni hii tumeirekebisha na yote yale mliyoyasema ndio ambayo tumeyachukua katika kutayarisha kabrasha hiyo. Kwa hiyo, sasa tunachokiomba ni idhini yenu ili kanuni hizi ziweze kutumika na Baraza letu liweze kufanya kazi yake vizuri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutoa hoja ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waweze kupitisha kanuni yetu hii. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa baada ya ufafanuzi aliofanya Mhe. Waziri. Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na marekebisho haya ya kanuni pamoja na yale maelezo mazuri aliyoyasema Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Hii maana yake ni kwamba marekebisho ya rasimu hii iliyopendekezwa hapa yanakubalika, *subject* yale maelezo Mhe. Waziri aliyoyatoa kwa baadhi ya vipengele ambavyo afisi yetu itaviingiza katika maeneo yanayohusika baada ya marekebisho ya Waheshimiwa Wajumbe waliyotoa hapa.

Marekebisho yale yangekuwa ni mengi mno nilitaka niseme kwamba tungekwenda katika Kamati ya Baraza Zima tukapitisha kifungu baada ya kifungu, lakini inaonekana kimsingi Waheshimiwa Wajumbe tumekubaliana na marekebisho haya pamoja na yale Mhe. Waziri aliyoyakubali kutokana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hiyo, sasa nitamke rasmi kwamba kanuni hizi zimepitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Kabla ya kuahirisha shughuli zetu kuna matangazo mawili matatu naomba niyatoe. Waheshimiwa Wajumbe mara baada ya kusitisha shughuli zetu kwa leo naomba niwakumbushe Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala

kwamba kamati yao itaendelea na kazi mara baada ya kuondoka hapa katika chumba namba mbili ili kuendelea na kuuchambua ule mswada unaohusu Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, naomba wajumbe wote hao wa kamati hiyo wakutane katika chumba namba mbili ili kuendelea na shughuli yao ya kuuchambua mswada huo.

Jambo la pili, katika shughuli zetu za kesho kazi yetu itakuwa ni kujadili Hotuba ya Mhe. Rais ambayo aliitoa mwaka jana tarehe 11 Novemba na tukakubaliana kwamba itakuwa ni moja kati ya kazi ya Baraza hili ili hotuba ile kuipokea rasmi. Kwa hiyo, kesho hotuba hiyo itawasilishwa mezani ili Waheshimiwa Wajumbe tupate kuijadili.

Kwa maana hiyo basi, vitabu vya hotuba naelewa kwamba tayari tumeshagaiwa tuipitie na tujitayarishe kwa ajili ya majadiliano kesho. Kwa maana hiyo hiyo basi, vitabu hivyo tuje navyo ili visaidie wajumbe kutoa michango yao vizuri na kwa wepesi zaidi.

Tangazo la tatu tulikubaliana kwamba tutengeneze vitambulisho kwa ajili ya makosa yale na masuala mengine ya vitambulisho. Kwa hiyo, upigaji wa picha kwa ajili ya vitambulisho hivyo unaendelea hapo nje wapiga picha wetu wako tayari na nafikiri Waheshimiwa Wajumbe tumejitayarisha vizuri sana ili kuweza kupiga picha hiyo kwa kiasi vile tunavyopendelea kwa mujibu tulivyo tukiwa na vazi linalokubalika na Baraza.

Haitapendeza kurudi ukenda ukavaa kitenge, tunataka tupige picha ambayo inaonesha huyu ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, mavazi yale ambayo yametajwa ndani ya kanuni ni vizuri ndio mavazi ya kupigia picha hayo. Haya tuliyovaa leo yanakubalika, kwa hiyo mtu akiona sasa amekaa vyema zaidi basi wale ambao hawajadiriki kufanya hivyo kupiga picha, basi picha itakuwa inaendelea hapo nje. Nafikiri hayo ndio matangazo kwa leo.

Shughuli yetu kwa leo inamalizika hapa, kimsingi jioni hatutakuwa na shughuli yoyote ili kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wajumbe kwenda kupitia ile hotuba ya Mhe. Rais ambayo kesho itajadiliwa na vile vile kwa kamati kuendelea na shughuli yake ya kuchambua mswada ule uliobaki wa Utumishi wa Umma.

Hivi Katibu kuna haja ya kumwambia Mhe. Waziri atoe hoja ya kuahirisha mpaka kesho kwa kuwa jioni hatuji.

Katibu: Taratibu za kanuni zinasema kama shughuli zinamalizika unaahirisha tu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kwa maana haya mambo ya kanuni yana matatizo yake, sasa ilikuwa niende kwenye *think tank* yangu hapa ambayo ndio hii meza ya chini hapo. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa kazi nzuri tuliyofanya leo asubuhi na naomba sasa nichukue nafasi hii kuahirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 20/01/2011 saa 3:00 za asubuhi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 5:54 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 20/01/2011 saa 3:00 asubuhi)